epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Alhamisi Mei 16, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581678

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**TEN HAG KUTOAGA MANCHESTER UTD**

# Matumbo joto uteuzi CHADEMA

• **Uongozi** wa chama wasema "ukikatwa..." *Endelea ukurasa 3*



John Heche



Joseph Mbilinyi 'Sugu'



Godbless Lema



Mchungaji Peter Msigwa



Ezekiel Wenje


UKURASA WA 2

**KAMERA ZA AKILI BANDIA KUFUNGWA MAENEO MAALUM KUNASA WAHALIFU**



UKURASA WA 5


**WATAFITI WAANIKA MBINU TANO ZA KUTOKOMEZA UGONJWA MALARIA**



UKURASA WA 5&8

INTANETI KUSUASUA

**WANAOOMBA AJIRA POLISI WAONGEZWA MUDA, WASITISHWA VISA UBALOZINI**



## Sababu aliyelala, kula hotelini kwa mil. 21/- kuachiwa huru

UK.2

## CAG afukua shida utoaji mikopo Z'bar

UKURASA 17

**MICHEZO** NYOTA WA MAZEMBE ATUA YANGA SC UK.24

**KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman (kushoto), wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya Kupikia, jijini Paris, Ufaransa juzi. Kampuni hiyo, imeahidi kumuunga mkono Rais, katika utekelezaji mzuri wa mpango wa upikaji safi nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sababu aliyelala, kula hotelini kwa milioni 21/- kuachiwa huru

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Goba kwa Kulangwa, Dennis Mfumbulwa (44), aliyeshtakiwa kwa kulala na kula siku 23 katika Hoteli ya Serena, jijini Dar es Salaam, na kutokulipa gharama za Sh. milioni 21.4 ameachiwa huru.

Mahakama ya Mwanzo ya Kariakoo imemwachia Mfumbulwa kwa sababu hakuna ushahidi unaoonyesha kwamba kosa hilo ni la jinai bali ni madai. Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Gladness Njau, baada ya kusikiliza ushahidi wa Meneja Uhusiano wa hoteli hiyo, Desdery Dotto, na kufikia uamuzi huo.

Hakimu Njau alisema baada ya kupitia ushahidi, hakuna sehemu inayoonyesha kwamba ni kesi ya jinai.

"Hakuna ushahidi unaothibitisha shtaka kwamba ni la jinai. Inaonekana asili ya hili shauri ni la madai na si jinai, kwa hiyo mahakama inamwachia huru," alisema Hakimu Njau huku akiongeza kuwa iwapo mlalamikaji ataona inafaa, amfungulie kesi ya madai.

Dotto alidai kuwa Mfumbulwa alikuwa anapata huduma ya malazi na chakula katika hoteli hiyo kisha akatoweka. Meneja huyo akiwa nje ya mahakama alisema yuko tayari kuendelea na kesi hiyo.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Karani Aurelia Bahati alidai kuwa mshtakiwa alitenda makosa hayo kati ya Machi 6,2022 hadi Machi 28,2024.

Ilidaiwa kuwa kwa nyakati tofauti katika Hoteli ya Serena, Mtaa wa Ohio, Ilala mkoani Dar es Salaam, mshtakiwa alijipatia huduma ya malazi na chakula yenye thamani ya Sh. 21,491,866.97 bila kulipa na hatimaye kutoweka huku akijua kuwa kitendo hicho ni kinyume cha sheria.

Hata hivyo, mshtakiwa baada ya kusomewa mashtaka yanayomkabili alikana kutenda kosa hilo.

# Kamera zenye akili bandia kufungwa maeneo maalum

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema itafunga kamera kwenye maeneo maalum nchini ili kunasa wahalifu.

Maeneo hayo ni pamoja na ya viwanda, biashara, mikusanyiko ya umma, barabara za miji, hoteli na huduma za jamii.

Ni mkakati uliobainishwa jana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni alipowasilisha bungeni jana makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Alisema mkakati huo utatekelezwa kupitia Mradi wa Miji Salama unaolenga kuboresha mifumo ya usalama nchini kwa kutumia teknolojia za kisasa ili kuhakikisha usalama wa watu na mali zao unaimarishwa.

"Katika utekelezaji mradi huo, jumla ya kamera 6,500 zenye teknolojia ya akili bandia zinatarajiwa kufungwa katika maeneo ya viwanda, biashara, mikusanyiko ya umma, barabara za miji, hoteli na huduma za jamii.

"Mradi utaanza kutekelezwa mwaka 2024/25 katika majiji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. Utatekelezwa kwa mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani 145,200,000 kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE)," alisema.

Waziri Masauni alitaja maeneo mengine ya kipaumbele mwaka ujao wa fedha ni pamoja na kuendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai; kukamilisha, kuendeleza na kuanza ujenzi wa ofisi, vituo na makazi ya askari na kuongeza vitendea kazi vya kisasa katika kutoa huduma ikiwamo magari, pikipiki, boti na helkopta.

Alisema wizara yake pia itaanza utekelezaji miradi ya kimkakati ikiwamo Mradi wa Ukaguzi wa Magari wa Lazima, Mradi wa Udhibiti wa Barabara Kuu.

Masauni alitaja maeneo mengine ni kuimarisha mifumo na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji huduma na ukusanyaji wa maduhuli ya serikali.

Vilevile, alitaja kipaumbele cha kutumia nishati safi kwenye magereza, kambi za wakimbizi na vyuo vilivyo chini ya wizara hiyo, ikiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Alieleza kuwa katika kutekeleza mradi wa ukaguzi wa magari wa lazima, watahuisha mfumo wa ukaguzi wa vyombo vya moto nchini ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na kupunguza ajali za barabarani zinazochangiwa na ubovu wa vyombo vya moto.

"Gharama za mradi ni Dola za Marakeni milioni 112 sawa na Sh. bilioni 286.16, Waziri Masauni alisema. Utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano.

Utekelezaji mradi huu utasaidia kupunguza ajali na kuongeza ufanisi kama ilivyo azma ya Rais Samia Suluhu Hassan, Rais ya kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa na lenye kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Tutatekeleza pia Mradi wa Udhibiti wa Barabara Kuu unaolenga kusimamia watumiaji barabara kuu kupitia mifumo ya kidijiti."

Alisema mradi utawezesha kufuatilia mienendo ya madereva na kutoa taarifa za hali za usalama wa barabara kwa watumiaji ili kuchukua tahadhari.

Waziri Masauni alisema jumla ya Sh. bilioni 36.006 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari 181 na Sh. bilioni 18.139 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kijeshi.

Alisema wizara kupitia Jeshi la Polisi itatekeleza miradi ya kipaumbele ambayo ni pamoja na kumalizia ujenzi wa Vituo vya Polisi Daraja "C" vya Msomera, Tanga - Sh. milioni 220; Tumbatu, Kaskazini Unguja - Sh. milioni 209.454; na kuendeleza ujenzi wa Vituo vya Polisi Daraja "B" vya Bariadi, Simiyu - Sh. milioni 220; Masasi, Mtwara - Sh. milioni 798; Mvomero, Morogoro - Sh. milioni 90.251; na Mwera, Mjini Magharibi - Sh. milioni 50.

Pia alisema Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa zitajenga vituo vipya vya polisi kata 12 na kukamilisha ujenzi wa vituo vya polisi kata 77 vilivyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi.

Alitaja miradi mingine ni kukamilisha ujenzi wa uzio wa nyumba za Makamishna wa Polisi - Dodoma awamu ya pili - Sh. milioni 344.213; ujenzi wa Rest House, Arusha - Sh. milioni 139; kumalizia ujenzi wa ghorofa la kuishi familia 12 Buyekera, Kagera - Sh. bilioni moja.

Pia alisema watamalizia ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa Manyara - Sh. milioni 800; na ujenzi wa nyumba nne za kuishi askari katika Kambi ya Finya, Kaskazini Pemba - Sh. milioni 250.

Alisema miradi mingine itakayotekelezwa ni ujenzi wa nyumba nne za kuishi askari Kambi ya Mfikiwa, Kusini Pemba - Sh. milioni 250; ujenzi wa nyumba mbili za kuishi askari katika kisiwa cha Tumbatu, Kaskazini Unguja - Sh. milioni 250; ujenzi wa Kituo cha Polisi Bububu, Mjini Magharibi - Sh. milioni 250; na ujenzi wa maghorofa manane ya kuishi askari na familia zao Dodoma - Sh. bilioni 7.785.

### KUPANDA VYEO

Waziri Masauni alieleza kuwa kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, wizara imepandisha vyeo jumla ya watumishi 9,397 katika ngazi mbalimbali za uongozi ambapo kwa Jeshi la Polisi watumishi 7,239 wamepandishwa vyeo.

Kwa mwaka 2024/25, wizara itawapandisha vyeo jumla ya watumishi 26,876, wakiwamo 20,009 wa Jeshi la Polisi. Wizara pia inatarajia kuajiri watumishi 4,857; wakiwamo 114 wa makao makuu ya wizara, 3,068 wa Jeshi la Polisi, 613 Jeshi la Magereza, 425 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 517 Jeshi la Uhamiaji na 120 wa NIDA.

Masauni alisema kuwa katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, jumla ya matukio 1,463 ya ajali za barabarani yaliripotiwa kulinganishwa na matukio 1,283 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hivyo, kuna ongezeko la matukio 180 sawa na asilimia 12.

Alisema ajali zilizosababisha vifo zilikuwa ni 985 kulinganishwa na 842 zilizotokea kipindi kama hicho mwaka 2022/23, ikiwa ni ongezeko la matukio 143 sawa na asilimia 14.

Alisema watu 1,408 walipoteza maisha kulinganishwa na watu 1,289 waliopoteza maisha mwaka 2022/23; ongezeko la vifo vya watu 119 sawa na asilimia tisa.

Alisema watu 2,166 walijeruhiwa kulinganishwa na watu 1,893 waliojeruhiwa kwa ajali mwaka 2022/23. Ni ongezeko la watu 273 sawa na asilimia 14.

Waziri huyo lisema katika kipindi hicho, makosa ya ukatili wa kijinsia yameongezeka. Yaliyoripotiwa vituo vya polisi yalikuwa 24,535 kulinganishwa na makosa 21,317 ya kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

Ili kutekeleza majukumu kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Masauni aliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 1.712 kwa ajili ya mapato na matumizi ya wizara yake.

Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 551.583 ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo, Sh. bilioni 870.429 ni za mishahara na Sh. bilioni 289.698 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

HABARI KITAIFA

# Matumbo joto uteuzi CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema majina ya watiania katika nafasi mbalimbali za uongozi kwenye Kanda yanatarajiwa kutangazwa wakati wowote huku kikiwataka watakaokatwa kukubali matokeo.

Mchujo wa watiania hao ulimalizika usiku wa kumkia jana.

Juzi, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema (pichani), alisema watiania watakaokatwa inabidi wakubali matokeo kwa kuwa zipo kazi nyingine za chama watakazoendelea kufanya.

"Tukikamilisha uteuzi tutawajulisha ambao wameteuliwa na ambao hawakuteuliwa. Maana ya usaili ni kwamba tuna vigezo vyetu kwa mujibu wa katiba na kanuni yetu, ni sifa gani viongozi wa ngazi gani wanapaswa kuwa nayo," alisema Mrema.

"Kama mtu akikutwa hana hizo sifa, basi moja kwa moja anaweza akaenguliwa, atashauriwa atumikie majukumu mengine kwa sababu bado ni chama kimoja, nafasi ni chache, wanachama wote hawawezi kuwa viongozi."

Mmoja wa maofisa wa chama hicho aliliambia gazeti hili kuwa majina ya wasailiwa yanatarajiwa kutolewa wakati wowote ndani ya siku mbili kuanzia jana.

"Jana (juzi), Kamati Kuu ilimaliza kazi ya kuchuja majina ya wasailiwa wote na sasa kinachosubiriwa ni kutoa majina ya watakaoteuliwa ambayo wakati wowote yatatolewa, kama sio kupitia mkutano na waandishi wa habari, lakini itatolewa taarifa kwa umma," alisema.

Kwa mujibu wa Mrema, kanuni ya 7.5 ya chama hicho, yenye vipengele zaidi ya 13 inaeleza sifa ambazo kila mgombea kulingana na nafasi yake anatakiwa kuwa nazo.

"Nafasi ya Mwenyekiti inaeleza anatakiwa awe na sifa gani, Katibu, Mwenezi na nyinginezo ziko kwenye kanuni za chama," alisema Mrema.

Alisema watiania waliosailiwa katika kanda hizo nne ni 136, wanao tiania kwenye nafasi za mabaraza na za chama.

Awali, kikao hicho kilipangwa kifanyike siku tatu, lakini kilifanyika kwa siku nne.



"Awali, kikao chetu kilipangwa kifanyike kwa siku tatu, lakini Kamati Kuu ililazimika kukisogeza mbele kwa siku moja. Katika kikao hiki tumekuwa na ajenda nyingi mojawapo ikiwa kupokea taarifa ya uchaguzi wa ngazi za mikoa, wilaya, majimbo, kata, mitaa, vijiji na misingi kwa nchi nzima pamoja na kufanya uteuzi kwa wagombea wa kanda nne za Victoria, Serengeti, Magharibi na Nyasa," alisema Mrema.

Mada nyingine zilizojadiliwa katika kikao hicho cha Kamati Kuu ni pamoja na kupokea taarifa ya chaguzi, kupokea tathmini ya maandamano ya awamu ya kwanza ya mikoa na kuweka mwelekeo wa awamu ya pili ya maandamano na kufanya usaili wa kuteua wagombea nafasi za uongozi katika kanda nne.

Katika siku zote hizo nne za kikao cha Kamati Kuu, yapo mambo mengi yaliyokuwa yanajitokeza hususani kwa watiania waliokuwa wameweka kambi makao makuu ya chama hicho Mikocheni kwa siku mbili kusubiri kusailiwa ikiwamo majigambo.

Miongoni mwa majigambo yalikuwa ya kutunishiana 'misuli' ya nani anaweza kukatwa na nani anaweza kubaki wakihusisha historia zao katika eneo la nidhamu ndani na nje ya chama, misimamo yao na namna ya kushinda mitego mbalimbali inayohusu hujuma za chama chao hasa kuelekea kipindi cha uchaguzi.

Kadhalika, wapo baadhi walisikika wakiwa na mazungumzo ya kutamani wasikie kauli ya chama kuhusu kile kinachodaiwa kuwapo fedha chafu ndani ya chama hicho hasa katika maeneo yanayofanya uchaguzi.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara Mei 2, mwaka huu, Makamu Mwenyekiti Bara wa chama hicho, Tundu Lissu, alitamka hadharani kwamba ndani ya chama hicho kuna harufu ya fedha chafu ambazo zimemwagwa kuvuruga uchaguzi.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions ndio uende **"pay via mobile"**. Itakuletea maelekezo namna ya kulipa kwa simu kulingana na mtandao unaotumia.
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia
6. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

7. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-6



Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Waitara aibua madai mazito TRA Sirari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara, ameibua madai bungeni kuhusu ukusanyaji kodi kusababisha madhara eneo la Sirari, ikiwamo kijana mwenye bidhaa za plastiki kufariki dunia kutokana na kusukumwa kwenye mtaro na gari lililokuwa linatumiwa na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Akiomba mwongozo kwa kiti kwa kutumia Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Waitara alisema wakati anapata majibu ya serikali kwenye swali la nyongeza la swali lake la msingi la 344 alieleza utaratibu unaotumika kukusanya kodi kwenye eneo hilo umesababisha madhara hayo.

Alisema gari hilo lilikuwa likimkimbiza kijana huyo na kumsukuma kwenye mtaro na kufariki dunia, tunashuhudia wengine wakipigwa hadi risasi.

"Nilidhani ingependeza sana kauli ya serikali, je, ni sahihi kutafuta kodi ya serikali kwa njia ya damu? Yaani unakusanya kodi kwa kuua watu na sio mara moja watu wetu wa TRA kule Sirari wana mipini ya jembe wanapiga vijana wa Tarime nadhani serikali itoe kauli juu ya hili ili wachukue kodi kistaarabu na kama kuna mtu ana magendo achukuliwe hatua bila kujenga chuki kwa watu wetu dhidi ya vyombo yetu vya ulinzi na usalama na TRA," alisema.

Akijibu mwongozo huo, Mwenyekiti wa Bunge, Deodatus Mwanyika alisema; "Mheshimiwa Waitara hapa kiti hakina nyaraka yoyote ya kuhakiki hilo jambo unalosema kwa hiyo nalipokea na tutarudi kwenu au kwako kadri kanuni zinavyoturuhusu."

Hata hivyo, alimshauri Mbunge kupeleka swali la msingi ili kupata majibu ya serikali.

Awali, katika swali lake la msingi, Mbunge huyo alihoji lini serikali itaweka kituo kidogo cha forodha katika Kata ya Itiryo/Bikonge pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa kupata bidhaa kutoka Kenya.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alisema kituo cha forodha Kata ya Itiryo/Bikonge ni miongoni mwa vituo tarajiwa vya forodha vitakavyofanyiwa tathmini na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika mwaka 2024/25.

"Tathmini itafanyika kwa kuzingatia vigezo mahsusi ikiwamo uwiano wa gharama za ukusanyaji wa mapato na kiwango cha kodi kinachotarajiwa kukusanywa katika kituo hicho. Endapo kituo hicho kitakidhi vigezo, mchakato wa uanzishaji wake utaanza kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema.

Aliwaelekeza wafanyabiashara wanaotumia mpaka wa Tanzania na Kenya uliopo Kata ya Itiryo/Bikonge, kuendelea kutumia vituo rasmi vya forodha vya karibu ikiwamo Kituo cha Forodha cha Sirari ili kurahisisha zoezi la ulipaji kodi na ukusanyaji wa mapato ya serikali.



Mkurugenzi Idara ya Afrika wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Ali Bujiku (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya Miaka 61 ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika Mei 25, mwaka huu. Kushoto ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa Wizara hiyo, Balozi Mindi Kasiga na Balozi wa Comoro nchini, Dk. Ahmada El Badaoui Mohamed. **PICHA: JUMANNE JUMA**

SIKU YA FAMILIA

## Gwajima ataka wazazi kufanya vikao kubaini ukatili

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wazazi na walezi kuwa na utaratibu wa kufanya vikao vya familia ambavyo vitawasaidia kuzungumza na watoto wao ili kubaini vitendo vya ukatili wa kijinsia wanavyofanyiwa na jamaa wa karibu.

Aidha, Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimeishauri serikali kutunga sera ya familia ili kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, udhalilishaji watu na vifo vitokanavyo na matukio hayo.

Dk. Gwajima amesema anatamani kutembelea kila nyumba nchini ili kuona mihutasari ya vikao vya familia vinavyofanywa.

Alibainisha hayo jana jijini hapa kwenye maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani na uzinduzi wa Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto awamu ya pili (MTAKUWWA II).

Alisema moja kati ya sababu zinaonekana kuchangia kwa kiasi kikubwa ukatili wa kijinsia kwa watoto ni wazazi na walezi kutokuwa na muda wa kuzungumza na familia zao na kuweka muda mwingi kwenye utafutaji wa maisha.

"Familia zipaswa kufanya vikao wewe baba ndiye rais wa familia na mke wako ndiye waziri mkuu na watoto wenu ndiyo wabunge hivyo mnapaswa kuweka utaratibu wa kufanya vikao vya familia kuzunguza, ili kubaini mambo yanayo wakabili watoto na kuyafanyia kazi natamani hata ningekuwa na uwezo wa kutembelea kila familia ili niweze kudai mikhutasari ya vikao vya familia," alisema.

Alisema tofauti za wazazi hazipaswi kuathiri malezi na makuzi ya watoto na kukimbilia mitaani.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema wizara yake itatoa ushirikiano wa kutosha kutekeleza Mpango kazi huo.

Vilevile, Mchengerwa aliwataka wakuu wa mikoa, wilaya pamoja na wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuweka mikakati ya kudhibiti vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto nchini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Theopistha Mallya, alisema vitendo vingi vya ukatili kwa watoto vinafanywa na watu wa karibu na kwamba wazazi wanapaswa kuacha tabia ya kulaza chumba kimoja watoto wao na wageni.

### TAMWA YATAKA SHERIA

Akizungumza katika maadhimisho ya siku ya familia duniani yalioandaliwa na chama hicho kwa kushirikiana na Shirika la kuwezesha Jamii yani Society Empowerment Organ (SEO), Mkurugenzi wa TAMWA, Dk. Rose Reuben alisema sera hiyo itasaidia kuhuisha familia zinazodhorota kutokana na matukio hayo.

Alisema ripoti mbalimbali zinaonyesha kuwapo ongezeko la ukatili wa jinsia kwa wanawake na wanaume, ukatili kwa watoto na ongezeko la nyumba zinazoendeshwa na mzazi mmoja kwa sababu moja ama nyingine.

Mkurugenzi wa SEO, Upendo Mwichande, alisema sera hiyo ni muhimu kwa kuwa itaweka uzito wa umuhimu wa taasisi ya familia kwa wanajamii na kwa serikali kuongeza vipaumbele vyake katika mipango na matumizi katika taasisi hii.

***Imeandikwa na Paul Mabeja (DODOMA) na Jenifer Gilla (DAR)***

## Timu mapitio mishahara sekta binafsi kuleta taarifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa timu ya mapitio ya kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi, imeanza kazi Aprili mwaka huu na itakapokamilisha taarifa yake itawasilishwa bungeni.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Deogratius Ndejembi alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo.

Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kuhakikisha kima cha chini cha mshahara kinakuwa Sh. 370,000 kwa sekta binafsi. Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema timu hiyo inahusisha Utatu yaani serikali, Chama cha Waajiri (ATE) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA ) na itakapokamilisha majibu hayo yatapelekwa bungeni.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuwapandishia mishahara wafanyakazi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete akijibu swali hilo, alisema ni jukumu la serikali kupandisha mishahara ya watumishi wake na itaendelea kupandisha mishahara ya watumishi.

"Mathalani: Julai, 2022 Serikali iliongeza mshahara wa kima cha chini kwa watumishi wa umma kwa asilimia 23.3, kutoka Sh.300,000 hadi 370,000 kwa mwezi. Nyongeza hiyo ya mishahara ilitolewa pia kwa watumishi wote wa umma kwa viwango tofauti tofauti kulingana na viwango vya mishahara ya watumishi," alisema.

## Daktari aonya ongezeko wagonjwa shinikizo la damu

**Na Waandishi Wetu**

WATU wazima watatu hadi watano kati ya 10 nchini, wanaugua shinikizo la juu la damu, imebainika.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) taasisi hiyo, Dk. Tulizo Shemu, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kuelekea kilele cha Siku ya Shinikizo la Juu la Damu Duniani inayoadhimishwa Mei 17, kila mwaka, kuna idadi kubwa ya wagonjwa wa shinikizo la damu ambao hawafahamu hali zao.

"Duniani takwimu zinaonyesha kuna watu bilioni 1.2 wana shinikizo la juu la damu. Kwa kawaida presha kama tulivyozoea kuita, kiwango cha kawaida ni 120/80 lakini baadhi ya watu wana kiwango cha juu.

"Tanzania watu watatu hadi watano watu wazima wana presha. Kwa bahati mbaya zaidi ya asilimia 60 hawajitambui, tumegundua asilimia 30 tu na asilimia tisa tu wanapata matibabu mbalimbali," alisema Dk. Shemu.

Kuhusu dalili mahsusi za ugonjwa huo, Dk. Shemu alisema ziko tofauti kama vile, maumivu ya kichwa, kifua, mapigo ya moyo kwenda kasi na uoni hafifu.

"Kwa asilimia kubwa ugonjwa hauna dalili maalumu ndiyo maana tunashauri watu wapime. Ujumbe wa mwaka huu ni 'Zifahamu Tarakimu Zako za Shinikizo la Damu'," alibainisha. Alisema wataalamu wa taasisi hiyo watatoa huduma za vipimo na matibabu bure, kuanzia leo hadi kesho kwa watoto na watu wazima.

Pia alisema watapeleka wataalamu wa lishe ambao watatoa elimu ya lishe bora ili kuwapa wananchi uelewa na kufuata mtindo bora wa maisha, utakaowasaidia kuondokana na matatizo ya moyo.

TATIZO LA INTANETI

# Wanaoomba ajira polisi waongezewa siku tano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeongeza siku tano za kuomba ajira zilizotangazwa na Jeshi la Polisi kutokana na ukosefu wa intaneti huku ikieleza upatikanaji wa huduma hiyo umeendelea kuimarika.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alitoa kauli hiyo jana bungeni kutokana na mwongozo ulioombwa na Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga kwa kutumia kanuni ya 54 ili kutoa jambo la dharura.

Katika maelezo yake, Mbunge huyo aliomba bunge lisimamishe shughuli zake ili kujadili suala la ukosefu wa intaneti nchini ambalo limesababisha vijana wengi kushindwa kuingia kwenye mtandao wa polisi kuomba ajira hizo.

"Kipengele cha pili cha tangazo kinasema waombaji watume maombi kwa mfumo wa ajira wa Jeshi la Polisi, Mheshimiwa Mwenyekiti ukienda kwenye mfumo huu kutokana na tatizo la kimtandao vijana hawa wanapata shida, lakini tovuti hii imezidiwa kuingia vijana wengi inawezekana uwezo ni mdogo au mfumo haufanyi kazi vizuri, naomba mwongozo wako vijana huko wapo kwenye presha na kesho (leo) ni mwisho," alisema.

Masauni akitoa ufafanuzi alisema: "Hata sisi serikali tumeliona hilo jana tulikaa timu ya wizara na jeshi la polisi na tukakubaliana kwamba tuongeze siku tano, hivyo vijana waendelee kuchangamkia fursa ya kuwasilisha maombi yao."

Alisema siku hizo tano zinaanza kuhesabiwa baada ya siku ya mwisho ya tangazo iliyokuwa imetangazwa awali.

"Tutakaa na Waziri wa Habari kuona hali inavyokwenda kama itakuwa mbaya tutaangalia namna ya kufanya," alisema.

Hata hivyo, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema hadi jana zaidi ya asilimia 80 ya mtandao umerudi kwenye hali yake na inategemewa kuendelea kuimarika zaidi.

"Vijana waendelee kuomba mimi naamini serikali ya awamu ya sita ni sikivu itaangalia hali itakavyokuwa sisi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tutafanya tena tathmini kuona namna mtandao unavyofanya kazi halafu tutashauriana kuchukua hatua namna ya kusonga mbele pamoja," alisema.

Mwenyekiti wa Bunge, Deodatus Mwanyika, alitaka serikali iendelee kushughulikia suala hilo na kutoa taarifa kadri hali inavyokwenda.



Polisi Kata ya Ruanda, wilayani Mbozi mkoani Songwe, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Happy Lumbe, akitoa elimu ya madhara ya kujichukulia sheria mkononi kwa waendesha pikipiki maarufu bodaboda wa kijiwe cha Mtakuja Njiapanda ya Iyula, Kitongoji cha Luwemba, mapema wiki hii. **PICHA: ISSA MWADANGALA**

# Watafiti waanika mbinu tano kutokomeza malaria

**Na Gwamaka Alipipi**

WATAFITI wa ugonjwa wa malaria wametaja mbinu tano ambazo Tanzania inapaswa kuzitumia katika kuutokomeza ugonjwa wa malaria, mojawapo ni kuongeza ufuatiliaji na kujua maeneo ugonjwa huo ulipo.

Walitaja mbinu hizo jana jijini Dar es Salaam wakati wa Mkutano wa 32 wa Mwaka wa Kisayansi, ulioandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMRI), kwa kushirikiana na watalaamu wa magonjwa, watafiti, wanasayansi kutoka taasisi mbalimbali.

Mtafiti Mwandamizi wa NIMRI Kituo cha Amani mkoani Tanga, Dk. Patrick Tungu, alisema Tanzania ina njia bora za kupambana na maambukizi ya malaria lakini tatizo liko katika kasi ya kutokomeza.

"Ukiangalia lengo la serikali ni ifikapo mwaka 2030 nchi iwe imeondokana na malaria. Hadi sasa tumebakiza miaka sita tu kufika mwaka 2030. Tunakwenda taratibu sana katika kufikia malengo," alisema Dk. Tungu.

Alisema kunapaswa kuwapo ushirikiano wa mihimili mitatu ambayo ni mapambano dhidi ya wadudu, vimelea vya malaria na kuongeza ufuatiliaji wa ugonjwa.

Dk. Tungu pia alisema serikali inapaswa kujielekeza katika kudhibiti mbu wote wanaoeneza malaria ndani na nje ya nyumba kuliko kupambana na mbu aliyeko ndani pekee.

"Mbinu zetu ni kudhibiti mdudu (mbu) anayeuma ndani ndiyo maana tunahimiza watu watumie chandarua kilicho na dawa. tunamsahau mbu aliyeko nje ya nyumba. Sasa tunapaswa kuwadhibiti wote," alisema.

Dk. Tungu alisema pia serikali inapaswa kudhibiti mazalia ya mbu, kutumia chanjo ambazo zimeonyesha mafanikio hususani kwa watoto walio chini ya miaka mitano.

Naye Mtaalamu wa tabia za mbu na Meneja wa NIMRI Kituo cha Dodoma, Dk. Basiliana Emid, alisema tatizo linaloikwamisha Tanzania kutokomeza ugonjwa wa malaria ni kutokuwepo kwa ushirikiano wa pamoja na kutounganishwa nguvu katika mapambano.

Pia alisema tatizo lingine ni kuwapo kwa majarida ya kitafiti ambayo yanakuwa na taarifa za kisayansi kuhusu mbu lakini hayaleti uamuzi ya namna ya kutokomeza.

Alitaja tatizo lingine ni kutokuwapo kwa fedha za kutosha ili kuyafikia maeneo yote ya Tanzania hususani vijijini.

Dk. Emin ambaye pia ni Mtafiti Mwandamizi Mkuu katika fani ya kisayansi ya kufuatlia mbu wanaouma binadamu na kusababisha magonjwa, alitaja kizingiti kingine ni jamii hususani wanaoishi vijijini kutoshirikishwa katika mapambano.

"Tunapaswa kuishirikisha jamii yote katika mapambano ya ugonjwa wa malaria kuanzia ngazi ya chini kabisa ambako wengi hawana vyombo vya habari. Wanapaswa kufikiwa kwa kupewa elimu ya namna ya kujikinga na maambukizi," alisema.

Dk. Basiliana alisema ili Tanzania ifikie malengo ya kutokomeza ugonjwa wa malaria kunapaswa kuwekwa nguvu katika kuangamiza mazalia ya mbu pamoja na viluivuli vya ugonjwa huo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu zaidi inahitajika katika mapambano dhidi ya saratani

**MARADHI** ya saratani yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku, hivyo kuwa janga la kidunia na tishio jipya kwa maisha ya wanadamu. Maradhi hayo kama vile saratani ya mlango wa kizazi kwa kinamama, tezi dume, saratani ya matiti, mapafu, ubongo yamekuwa mzigo mkubwa katika jamii hususan katika nchi zinazoendelea.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuwa mwaka 2022, takribani watu milioni 20 walibainika kuwa na maradhi hayo huku watu milioni 9.7 wakipoteza maisha. Taarifa hiyo ya miaka miwili iliyopita inabainisha kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la maradhi ya saratani duniani na kwamba ifikapo mwaka 2050, inakadiriwa kuwa watu milioni 35 watakuwa wamepatwa na maradhi hayo kama hali itaendelea kuwa kama ilivyo sasa.

Kwa nchi zinazoendelea zikiwamo za Afrika, hali inaelezwa kuwa mbaya zaidi na kwamba kuna hatari ya maradhi hayo kuongezeka kwa watu milioni moja kwa mwaka ifikapo mwaka 2030. Vifo vitokanavyo na maradhi hayo pia vinaelezwa kuwa vinaweza kuongezeka mara mbili ndani ya kipindi hicho

Taarifa hizo kwa Afrika, kwa mujibu wa WHO, zinaonyesha kuwa mwaka 2022, watu 882,882 waligundulika kuwa na saratani na kati ya hao takriban 574,000 walifariki dunia.

Kwa Tanzania takwimu si za kufurahisha kwa sababu inaelezwa kuwa wagonjwa wapya 40,000 hugundulika kila mwaka na vifo 27,000 hutokana na maradhi hayo. Aidha, imebainishwa kuwa saratani ya mlango wa kizazi ambayo huwakumba zaidi wanawake, ndiyo huongoza katika orodha ya maradhi hayo. Kutokana na takwimu hizo, hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa afya katika kupambana na maradhi hayo huku msisitizo mkubwa ukiwekwa katika kudhibiti na kuzuia maambukizi.

Kampeni hiyo ya kuzuia imekuwa ikienda sambamba na kuzuia maradhi yasiyo ya kuambukiza kama vile shinikizo la juu la damu, figo na moyo ambayo yamekuwa yakigharimu serikali fedha nyingi. Pamoja na jitihada zinazofanyika na serikali yakiwamo makongamano na mikutano mbalimbali kuhusu maradhi hayo, saratani ikiwamo, bado kuna tatizo kubwa hasa kwa jamii za vijijini kwa sababu wagonjwa wengi wanaofikishwa katika vituo vya matibabu, wanakuwa katika hatua za mwisho na wanakuwa wameathirika kwa kiwango kikubwa.

Wagonjwa wanaofikishwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) kwa ajili ya matibabu zaidi baada ya kutibiwa katika hospitali za rufani za mikoa na kanda, ni uthibitisho wa namna tatizo hilo lilivyo kubwa. Baadhi ya taarifa kutoka katika hospitali hizo ziliwahi kunukuliwa kuwa watu wanafikishwa wakiwa kwenye hatua ambazo inakuwa vigumu kwa kiasi kikubwa kupata tiba na baada ya muda mfupi hufariki dunia.

Ni vyema jitihada zikaongezwa katika kuhamasisha watu kujua afya zao mapema ili wanapobainika kuwa na matatizo, waanze kupata matibabu kwa wakati. Ni imani kwamba hatua hiyo itasaidia kupunguza ongezeko la vifo vitokanavyo na saratani, ikiwamo ya shingo ya kizazi.


Elimu zaidi inapaswa kupelekwa vijijini ambako tatizo limeanza kuwa kubwa na watu wamekuwa wakifikishwa hospitali kubwa kama Muhimbili wakiwa katika hatua za mwisho za ugonjwa. Aidha, katika utoaji wa elimu hiyo, jamii ikumbushwe kuhusu kubadili mitindo ya maisha hasa ulaji wa vyakula, unywaji pombe, uvutaji wa sigara na watoto wa kike wafundishwe kuhusu afya ya uzazi na kuacha kujamiiana katika umri mdogo kwa kuwa hiyo ni moja ya sababu ya ongezeko la saratani ya kizazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Elimu ya mlipakodi ianzie shule msingi, iwe tabia kuliko sheria

**KODI** ndio uhai wa serikali yoyote, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alipenda kukumbusha kila mara umuhimu wa kodi na nafasi yake kuiwezesha serikali, nayo ikatimiza majukumu yake kwa wananchi.

Mwananchi huyo katika jicho la awali, ana wajibu wa awali, kuwa mzalendo katika ulipaji kodi. Mwenendo huo unazaliwa na mwamko wa kuwajibikia kulipa kodi kwa hiari.

Kurejea uhalisia uliopo, kumekuwapo malalamiko kutoka kwa baadhi ya maofisa wa Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA), kuwa baadhi ya wafanyabiashara wanashindwa kutekeleza wajibu wao wa kulipa kodi.

Malalamiko hayo yanakuja pale wanapofika katika maduka ya baadhi ya wafanyabiashara hao, wanashuhudia matukio ya ama kukimbia au kutoroka mahali hapo, kila wanapowaona wafanyakazi wa TRA. Kushindwa kuyatekeleza majukumu yao, ni hali inayochangia maofisa tajwa, kufanya kazi katika mazingira magumu.

Hapo inazua hata maswali ya kimantiki, kwanini mtu akimbie wajibu wake akikwepa kodi halali na kwa matumizi ya serikali yake na mlengwa ni yeye?

Wapo baadhi ya wafanyabiashara ambao wanaona hakuna umuhimu wa kulipa kodi na baadhi yao, wanafika hatua ya mbali, kuwakimbia maofisa wa TRA, pale wanapowaona penye miradi yao kuwakagua, uwajibikaji wao katika kulipa kodi.

Iwe kushoto au kulia, ulipaji kodi ni muhimu na lazima ya asili, kwa maana nzuri tu kwa kila nchi, kutokana na makusanyo yanayopatikana, yanasaidia nchi kupiga hatua za maendeleo.

Ukweli ni kwamba, kila mfanyabiashara anastahili kulipa kodi na kufanya hivyo, kunachangia kuongeza maendeleo ya kitaifa, kutokana na mapato yanayokusanywa kila mwezi. Wajibu huo wa kulipa kodi unasonga mbali, kila mtu katika jamii hiyo anawajibika kulipa kodi hiyo,

Umuhimu wa ukusanyaji kodi, pia unasaidia serikali mapato yake sehemu husika kuongezeka, hata mtu akaona mazao yake ni maboresho katika huduma muhimu za kijamii, kama vile shule na zahanati.

Mapato hayo yanaweza kuongezeka maradufu, endapo jamii inayofanya biashara kuwa na elimu ya mlipakodi ikiwa na hoja na mantiki kichwani juu ya sababu inayomuongoza, hata akalipa kodi hiyo.

Wapo wanaofikiria kwamba kodi inatakiwa kulipwa na wafanyabiashara wakubwa tu, kumbe sio sahihi. Kodi kulipwa ina wajibu kwa kila mfanyabiashara na wengine wote wanaostahili kisheria, inakuwa lazima alipe kodi.

Mara zote serikali imekuwa ikitoa matangazo yanayohusu ulipaji wa kodi, na ufafanuzi wa kila namna, kodi hiyo inachangia kuwapo maendeleo ya jamii hii ya watoa kodi.

Serikali imekuwa ikishauri kila anayenunua bidhaa aombe risiti, kwa ajili ya manufaa kwa taifa pale inapotakiwa mtu kanunua kitu na kupatiwa risiti.

Katika mtazamo wangu, yawezekana jamii ina uelewa mdogo kuhusiana na masuala ya kodi na umuhimu wake au namna ya kuzingatia kanuni stahiki za kununua na kuwajibikia kodi hiyo, iingie serikalini.

Ukweli mara zote unabaki katika mstari kwamba, kodi inadumu kuwa akiba kumhudumia mtumiaji kesho na keshokutwa.

Najua wapo wanaokosea mantiki hiyo. Mathalan, wapo baadhi ya madereva wa magari ambao hununua mafuta katika vituo vya mafuta, lakini hawaombi risiti, kama alivyokuwa akisisitiza Hayati Rais Dk. John Magufuli.

Vilevile, wapo wanaonunua katika maduka makubwa nchini, lakini baadhi yao inapofika kipengele cha makubaliano, hadi wanaaga, hawaombi risiti, kwa kufanya hivyo ni kuikosesha serikali mapato.

Ndio maana kuna usemi unasisitizwa kila mara na TRA kwamba, kila mtu anaponunua kitu katika kituo cha mauzo, suala kuomba risiti, liwe ni 'lazima ya kudumu.'

Kwa kufanya hivyo, kila mtu atakuwa anaangukia katika umuhimu wa kulipa kodi. Hapo, inatakiwa elimu itolewe kuanzia shuleni, ambako elimu hiyo itawasaidia hata watoto kujua umuhimu wa kulipa kodi na umuhimu wa kuomba risiti.

Wakielewa wanafunzi wa madarasa ya chini mpaka wakifikia kuwa sehemu ya kundi kubwa la watu, watakuwa wanajua kudai risiti pale wanapofanya ununuzi wowote.

Kodi sehemu yoyote inatolewa na inachangia ukuaji wa maendeleo katika sehemu hiyo.

# Ndejembi aonya wasiowasilisha michango ya wafanyakazi NSSF

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema haitawavumilia waajiri wa sekta binafsi wanaokata michango ya wafanyakazi wao bila kuiwasilisha katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria na linawanyima haki wafanyakazi ambao wanashindwa kulipwa mafao yao kwa wakati wanapostaafu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Deogratius Ndejembi, alisema hayo wakati alipofanya ziara ya kikazi katika Ofisi za NSSF, jijini Dar es Salaam.

Aliwataka waajiri wenye tabia hiyo kuacha mara moja na watakaobainika hawatabaki salama na kuwa kumkata mfanyakazi fedha bila ya kuiwasilisha katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kunamletea usumbufu anapostaafu au ajira yake inapofikia ukomo kwa kushindwa kulipwa madai yao kwa wakati.

Alisema baadhi ya waajiri wanawasilisha kwenye mifuko asilimia kumi pekee ya mwajiriwa, lakini mchango wake wa asilimia kumi hauwasilishi ni kinyume cha Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo inamtaka mwajiri kumkata mfanyakazi asilimia zote ishirini.

Ndejembi alisema baadhi ya kero za wastaafu hususan za kusubiria mafao yao kwa muda mrefu zinasababishwa na waajiri kutowasilisha michango ya wafanyakazi wao kwa wakati na kusababisha adha kubwa kwa wastaafu na kudhani Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ndio inayowazungusha jambo ambalo muda mwingine sio kweli.

"Sasa tutakuwa wakali sana kwa waajiri wote ambao hawawasilishi michango kwa wakati kwani suala hilo ni kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha mifuko hii ya hifadhi ya jamii kuhakikisha kuwa waajiri wanawasilisha michango yao kwa wakati na hivyo tutasimamia jambo hili kwa ukali," alisema Ndejembi.

Aidha, alisema ameridhishwa NSSF kwa Mfuko kukua zaidi kuanzia kipindi ambacho Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani mwezi Machi 2021, thamani ya NSSF ilikuwa Sh. trilioni 4.8, lakini ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya awamu ya sita thamani imefikia trilioni 8.1.

"Huo ni ukuaji wa hali ya juu na hii inaonesha mafanikio makubwa ya serikali ya awamu ya sita na mafanikio ya utendaji mzuri ya Mfuko inayofanywa na Bodi ya Wadhamini, Menejimenti pamoja na Wafanyakazi wa NSSF," alisema Ndejembi.

Alisema kuna mambo ya msingi watu wanataka kuyaona yakitokea ikiwamo kuongeza nguvu ya huduma kwa mteja anayechangia katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwa anahudumiwa kwa wakati na changamoto zao zinaendelea kupokewa na kufanyiwa kazi.

Ndejembi amesema fedha za Watanzania zilizopo kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii atahakikisha zinawekezwa vizuri na kwa uadilifu kwenye miradi itakayoleta matokeo chanya na kurejesha fedha za wanachama ili kulipa mafao kwa wakati.

Mkurugenzi Mkuu, Masha Mshomba, amemshukuru waziri kwa kufanya ziara ya kikazi na kumwahidi kuwa yote aliyoelekeza na kuyawekea msisitizo watahakikisha wanayatekeleza.

Mshomba alisema NSSF inaendelea kuweka mkazo katika uboreshaji wa huduma kwa wateja na jambo hilo lipo katika Mpango Mkakati wa Mfuko, kwa sasa wameelekeza nguvu kwenye matumizi ya TEHAMA.




Balozi wa Qatar nchini, Fahad Rashid Al Mereki (katikati), akikabidhi msaada wa tende zilizoongezwa virutubisho kwa Mkurugenzi na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP), Sarah Gordon-Gibson (kushoto), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Dk. George Fasha. **PICHA: FAUSTINE FELICIAN**

## Mshtakiwa aomba amwone mke wake 'wakayajenge'

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Najim Mohamed ameomba mahakama imkutanishe na mke wake, Maryam Najim ili wazungumze mambo ya kifamilia kwa kuwa watoto wao wanatakiwa kwenda shuleni.

Wanandoa hao wanatuhumiwa kusafirisha dawa za kulevya zaidi ya kilogramu 3,000, zikiwa heroin kilogramu 882.71. Mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni mfanyakazi wa ndani, Juma Mbwana. Wote ni wakazi wa Kigamboni Kibugumo, Dar es Salaam.

Mohamed alitoa ombi hilo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa kwa njia ya mtandao. Ni baada ya Wakili wa Serikali, Eva Kassa kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kesi hiyo kuwa upelelezi haujakamilika.

Hakimu Lyamuya alimwuliza Mohamed kama ana chochote cha kuzungumza; naye alidai anacho, ndipo akapewa nafasi ya kuzungumza. Mohamed: Ninachoomba, ninaomba nikutanishwe na mke wangu ili tuzungumze mambo ya kifamilia kwa sababu watoto wanatakiwa kwenda shuleni.

Hakimu: Unajua wewe na mwenzio kwanini mmewekwa magereza tofauti ukiachana na utofauti wa kijinsia?

Mohamed: Hapana sijui.

Hakimu: Mimi ninamkumbuka mara ya kwanza kwamba mnakaa tofauti kutokana na sababu za upelelezi.

Baada ya hakimu kumweleza hayo, mshitakiwa alionekana kama kutokuelewa vizuri. Hata hivyo, hakimu alisema waachane na hayo, akaendelea na jambo lingine, akieleza kuwa wamepokea ombi hilo na watalifanyia kazi na majibu atapewa siku ya kesi yake itakapokuja kwa ajili ya kutajwa Mei 27, mwaka huu.

Awali Wakili wa Serikali Mwandamizi, Hemed Halfani, akisoma hati ya mashtaka alidai kuwa Desemba 15 mwaka huu, eneo la Kibugumo Shule, Kigamboni, Dar es Salaam, washtakiwa wote walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin kilogramu 882.71.

# Serikali kujenga vizimba kuwadhibiti mamba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa mikakati wa serikali kukabiliana na matukio ya mamba kujeruhi au kusababisha vifo kwa wananchi ikiwamo kujenga vizimba vya mfano.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dunstan Kitandula, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nkasi Kusini (CCM), Vincent Mbogo, aliyetaka kujua ni lini serikali itaweka wavu maeneo ambayo wananchi wanapoteza maisha.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kitandula, alikiri kuwa kumekuwapo na matukio ya mamba kujeruhi au kusababisha vifo vya watu hususan kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa maeneo yenye maziwa, mito na mabwawa.

Alisema katika kukabiliana na tatizo hilo, serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wadau imeandaa na inaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori.

Alibainisha kuwa moja ya malengo ya kimkakati ni kuwajengea uwezo wananchi kwa kuwapatia mafunzo ya mbinu za kujilinda na kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu akiwamo mamba.

"Katika kutekeleza mkakati huo, serikali imekwishajenga vizimba vya mfano kwa ajili ya kuzuia mamba katika baadhi ya maeneo hapa nchini," alisema.

Aidha, alisema serikali imeandaa Mpango wa kuendeleza ujenzi wa vizimba vya mfano vya kuzuia mamba katika maeneo mengine nchini yenye changamoto hiyo yakiwemo maeneo ya Ziwa Tanganyika kadri ya upatikanaji wa fedha.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji serikali kama ipo tayari kwenda kujenga vizimba vya mfano katika maeneo hatarishi ya katika kijiji cha Izimba.

Akijibu, Naibu Waziri alisema serikali ipo tayari kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

# Huduma za Visa zanasa kusuasua kwa intaneti

**Na Christina Mwakangale**

WATUMIAJI wa miamala ya kibenki pamoja na ving'amuzi kwa siku ya tatu mfululizo wamepata tatizo la intaneti huku Ubalozi wa Marekani nchini ukisitisha huduma kwa umma.

Kurasa za kijamii pamoja na ujumbe wa simu, zimeendelea kutoa taarifa kwa wateja wake wanaotumia huduma hizo, wakati Ubalozi wa Marekani nchini ukitangaza kutoa huduma ya dharura kwa raia wake pekee.

"Kutokana na changamoto za kimtandao nchini, Ubalozi wa Marekani itafunga huduma kwa umma. Miadi yote ya konseli kuanzia Mei 14 na 15, itafutwa na kupangwa baadaye. Kitengo cha konseli kitafunguliwa kama kawaida, kwa ajili ya kuchukua VISA na huduma za dharura kwa raia wa Kimarekani," ulieleza ukurasa wa Ubalozi huo katika mtandao wa Instagram.

Mmoja wa wateja, wanaotumia huduma za kibenki, aliimbia Nipashe jana kwamba, amepokea ujumbe unaosomeka: "Ndugu mteja kuna changamoto ya upatikanaji wa baadhi ya huduma zetu kutokana na hitilafu ya mtandao wetu, wanaendelea kushughulikia tatizo hili. Asante," ujumbe huo ulitumwa kwa mteja aliyejitambulisha kwa jina moja la Innocent.

Kadhalika, mtumiaji wa huduma ya king'amuzi, Baraka Haule, alisema ameshindwa kulipia kifurushi cha mwezi ambacho hujiunga kila baada ya siku 30.

"Nilipojitahidi kulipia huduma ya kifurushi, niletewa ujumbe mfupi wa maandishi kuwa huduma inakataa kulipia fedha katika mfumo, niwe mtulivu," alisema Haule.

Aidha, wasambazaji wakuu wa huduma ya intaneti, kwenda kwa taasisi binafsi na umma, ikiwamo za kibenki wanakadiria hali kutengemaa baada ya siku sita kuanzia Jumapili lilipoanza tatizo, baada ya utulivu na usalama baharini.

Anna Bruno, mkazi wa jijini Dar es Salaam, alisema hitilafu hiyo imemwathiri kwa sababu huagiza bidhaa kutoka nje na kujitangaza na kufanya mauzo kupitia mitandao ya kijamii huku kwa siku akiingiza kiasi kisichopungua Sh. 80,000.

"Mfano mimi ni kawaida kila siku kuuza bidhaa kupitia mtandaoni, nina kundi maalumu la kuungana na wateja wangu nilichoshangaa jana ujumbe kutoka kwa wateja uliingia kwa kusuasua nikadhani sina kifurushi, niliingiza mauzo kidogo kama Sh. 20,000 tu," alieleza.

Jason Ambross, mkazi wa Mwenge, Dar es Salaam, aliliambia gazeti hili kwamba kuna baadhi ya taarifa zinazotegemewa na wananchi kupatikana kwenye duka lake la 'steshenari', lakini tangu Jumapili hali ilikuwa tofauti.

"Ninatoa huduma za kutoa kopi, kuchapa, pia huwa naingia kwenye tovuti za umma kupata huduma, mfano taarifa ya 'loss report' siku hizi ni mtandaoni, wateja wangu hufika hapa, naifungua fomu kisha nawajazia taarifa, picha ikikamilika wanalipa Sh. 500 na hapo hapo serikali inaingiza Sh. 1,000 kupitia control namba, lakini tangu jana taarifa zinashuka taratibu sana au hazifunguki kabisa," aliongeza.



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana (kulia), akijadiliana jambo na Naibu wake, Jumanne Sagini katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bilioni 2.3/- kulinda haki za walaji

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Foundation for Civil Society (FCS) imeingia makubaliano na TradeMark Afrika kutekeleza mradi wa Sh. bilioni 2.3 wenye lengo la kulinda haki za walaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Justice Rutenge, alisema juzi Kinondoni, Dar es Salaam kuwa mradi huo wa miaka mitatu utazingatia pia makundi muhimu wakiwamo wenye ulemavu, wanawake na vijana.

Alisema baadhi ya kazi zitakazofanywa katika mradi huo ni kuwezesha wananchi kufahamu haki zao na kupaza sauti kuhakikisha wanapata bidhaa na huduma bora, sahihi na kwa wakati.

"Katika mradi huu tutafanya kazi na mabaraza ya walaji ambayo yamewekwa kisheria kwa kuyawezesha kuwa na uwezo wa kufanya kazi vizuri zaidi, Rutenge alisema, hivi sasa kwenye baraza, unakuta halina mfumo rasmi wa kupokea maoni kutoka kwa wananchi.

Mfano, juzi mtandao wa intaneti ulipokatika juzi, wananchi walipaswa kufahamu kuwa lipo baraza ambalo wangepeleka maoni yao, lakini mifumo bado haifanyi kazi vizuri. Kwa hiyo, wananchi watarajie kwamba tutasaidia kuboresha mifumo ya namna hiyo ifanye kazi vizuri."

Mkurugenzi Rutenge alisema mradi huo utasaidia kuwezesha makundi hayo maalum kuongeza fursa za biashara zenye ushindani.

"Na tunawajengea uwezo kuchangamkia fursa za kibiashara zenye ushindani ikiwamo kufanya zile ambazo zinatunza mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi," alisema Rutenge.

Mkurugenzi Mkazi wa TradeMark Afrika, Elibariki Shammy, alisema makundi mengine yatayojengwa uwezo katika mradi huo ni asasi za kiraria kwa kuzipa nguvu ya kushiriki kwenye masuala ya biashara kwa lengo la kuongeza bidhaa za Tanzania kuwa za kiushindani zaidi katika soko la kimataifa.

"Lakini kwenye makubaliano ya kikanda na kimataifa kwenye mashirika ya kibiashara, nyingi zinahitaji sana asasi za kiraia zijengewe uwezo wa kuzungumza masuala yanayowahusu ya masoko, kuzalisha bidhaa bora kwa afya ya walaji na ambazo zinapatikana kwa urahisi na bei ambazo ni sahihi.

"Kazi yetu kubwa ni kuhamasisha biashara na kutazama maeneo ambayo yanachangia kuleta vikwazo vya ufanyaji biashara ikiwamo mifumo, sera na sheria," alisema Shammy.

# Uzinduzi maboresho Daftari la Mpigakura, Julai mosi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uzinduzi wa zoezi la uboreshaji wa daftari la wapiga kura ambapo uzinduzi huo utafanyika Julai mosi, Mkoani Kigoma na unatarajiwa kuzinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, visiwani Zanzibar, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Jacobs Mwambegele, alisema siku hiyo ya uzinduzi pia uboreshaji utaanza katika mkoa huo na kuendelea katika mikoa mingine ya Katavi, Rukwa na Tabora.

Alisema kwa lengo la kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi, uboreshaji utafanyika kwenye mizunguko 13 itakayobainishwa na litaendeshwa kwa siku saba kwenye kila kituo cha kuandikisha wapiga kura.

Alisema watakaohusika kwenye uboreshaji huo wa daftari la kudumu la wapiga kura ni wapiga kura wapya raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 na zaidi, wapiga kura walioandikishwa awali na ambao wamehama kutoka mkoa au wilaya moja kwenda nyingine ili kuhamisha taarifa zao kutoka kata au jimbo walioandikishwa awali.

Alisema zoezi hilo litatoa fursa kwa wapiga kura walioandikishwa kurekebisha taarifa zao, kutoa kadi mpya kwa wapiga kura waliopoteza kazoo zao au kuharibika na kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya kuukana uraia wa Tanzania na kifo.





# Wodi maalum ya watoto njiti kuanzishwa rasmi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WIZARA ya Afya imetangaza kuanzisha rasmi wodi maalum za watoto wachanga, njiti na watakaozaliwa na uzito pungufu ili kusaidia kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano na vitokanavyo na uzazi.

Jana, mwakilishi wa wizara hiyo, Dk. Ismail Mtitu, alidokeza juu ya mpango huo wa serikali, wakati akikabidhi madaktari bingwa na bobezi 35 kwa Mkoa wa Manyara kwa ajili ya kutoa huduma za kibingwa kwa wiki moja.

Dk. Mtitu alisema serikali inahitaji angalau kufika mwaka 2025 hospitali zote za wilaya nchini ziwe zimeanzisha wodi za watoto wachanga kwa asilimia 80, ili kuendelea kupunguza vifo.

Aidha, alisema kwa mujibu wa Ripoti ya Viashiria vya Malaria ya Mwaka 2022 (TDHS-MIS), vifo vya watoto chini ya miaka mitano, vimepungua kwa asilimia 36 kutoka 67 kwa vizazi hai 1,000 hadi vifo 43 kwa vizazi hai 1,000.

Vilevile, Dk. Mtitu, alisema vifo vya watoto wachanga vinapungua kwa kasi ndogo kwa asilimia nne kutoka asilimia 25 kwa vizazi hai 1,000 hadi vifo 24 kwa vizazi hai 1,000.

"Ndiyo maana tunasisitiza uanzishwaji wa wodi maalum ya watoto wachanga, wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu," alisema Dk. Mtitu.

Pia alisema ripoti hiyo ilionyesha vifo vitokanavyo na uzazi na vya watoto wachanga vimepungua kwa asilimia 81 kutoka vifo 556 kati ya vizazi hai 100,000 mwaka 2015/2016 hadi vifo 104 kati ya vizazi hai 100,000 mwaka 2021/22.

Pia alisema mpango wa madaktari wa Dk. Samia, wanaotoa huduma za kibingwa na bobezi kila halmashauri mkoani Manyara, kwamba itapokea madaktari watano.

Alitaja madaktari watakaotoa huduma kuwa ni Daktari Bingwa wa Watoto Wachanga, Daktari Bingwa wa Upasuaji, Daktari Bingwa wa Usingizi, Daktari Bingwa wa Afya ya Uzazi, Daktari Bingwa wa Wajawazito na Wanawake na Daktari wa Magonjwa ya Ndani.

Daktari Bingwa wa Watoto wa Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza, Dk. Veronica Kaniki, alieleza kuwa uanzishwaji wa wodi za watoto wachanga ni muhimu.

Dk. Kaniki, alisema ni muhimu kwa kuwa zinapunguza vifo vya watoto wachanga na watoto njiti ambao zamani waliitwa kuwa siyo ridhiki.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, akiwapokea madaktari hao alisema kwa sasa madaktari bingwa na bobezi, wanawafuata wagonjwa mikoani na wilayani, tofauti na miaka ya zamani.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Rashid Mfaume, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu madaktari bingwa na bobezi kufika vijijini.



Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Tanga, Dastan Singano, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Pangani hivi karibuni, wakati akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi wa ujenzi wa barabara ya Tanga-Pangani yenye urefu wa kilomita 50 kwa kiwango cha lami ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 74. Kushoto Mwenyekiti wa Halmashauri ya Pangani, Akida Bahorera. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yataja chanzo cha kuenea kwa visumbufu vya mimea

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, amesema biashara za kimataifa kwa kiasi kikubwa zinaweza kuchangia kuingia na kuenea kwa visumbufu vya mimea na kusababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na mimea.

Alisema kutokana na ongezeko la idadi ya watu duniani, ili kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuongezeka kwa mwingiliano wa biashara za mazao na kulinda afya za mimea, kuna umuhimu wa kujenga mifumo imara ya kudhibiti afya ya mimea.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wadau mbalimbali wa sekta hiyo jijini Arusha kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Afya ya Mimea.

Alisema ili kupunguza athari za visumbufu hivyo ni wajibu kwa wadau kushirikiana na serikali kuchukua hatua mahususi za usimamizi wa usafi wa mimea, kufuata viwango na miongozo ya kimataifa, sheria na kanuni zinazosimamia afya ya mimea.

Aidha, Dk. Mweli, alisema serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwenye kilimo kwa kutenga fedha nyingi kwenye bajeti kwa ajili ya uendelezaji wa sekta hiyo.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, mimea ni msingi wa maisha duniani kwa kuwa inatoa chakula, dawa, hewa safi na huduma mbalimbali za mazingira.

Alisema afya ya mimea inakabiliwa na athari ya tishio la visumbufu hatarishi na mabadiliko ya tabianchi ambapo husababisha kuwapo kwa aina mbalimbali ya visumbufu ambavyo vinatoka kwenye mazingira yao ya asili.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), Prof. Joseph Ndunguru, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuikumbusha dunia kuweka umakini wa afya ya mimea ili kutokomeza maisha duni na umasikini kwa ajili ya kutilia mkazo umuhimu wa kulinda mimea.

Mwenyekiti wa Bodi ya TPHPA, Prof. Andrew Temu, alisema kwa sasa katika sekta ya kilimo kumekuwapo na maendeleo ya kasi ambayo yamechangia kukuza sekta hiyo kwa maslahi ya taifa.

Mwakilishi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mande Hosen, alisema shirika hilo, limekuwa likitoa msaada kwa mataifa mbalimbali duniani kuhakikisha binadamu wanakuwa salama na wenye furaha, ikiwamo kupata chakula cha kutosha kwa ajili ya kula na kufanya biashara kwa lengo la kuongeza kipato.

## Wabunifu 283 wagunduliwa, waendelezwa

**Na Getrude Mpezya,** ARUSHA

SERIKALI imesema mpaka sasa wabunifu 283 wamegunduliwa katika nyanja mbalimbali na kuwezeshwa bunifu zao.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Franklin Rwezimula, aliyasema hayo jijini Arusha jana wakati akizungumza na maofisa elimu kata.

Dk. Rwezimula, alikwenda kufungua mafunzo ya uanzishwaji wa madawati na majukwaa ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Alisema kutokana na mkakati huo serikali imeanza kuimarisha mifumo na utaratibu wa uboreshwaji wa mitaala mipya ili kutambua zaidi bunifu hizo.

"Kwa ulimwengu tunaoishi, huwezi kuikwepa sayansi na teknolojia ila tunachotakiwa kufanya ni kuwatambua wabunifu sehemu walipo kwa kuwafikia na kuendeleza ubunifu wao.


"Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kutekeleza ubunifu katika nyanja mbalimbali na mpaka sasa tumegundua bunifu zaidi ya 283 zilizobuniwa na Watanzania, huku bunifu 42 zikiwa zimeshaingia sokoni, kwa kupitia uhusiano hayo kutaongeza chachu ya ubunifu katika maeneo tofauti ya nchi yetu," alisema.

Dk. Rwezimula alisema kuwa washiriki wa mafunzo haya wanatakiwa kuanzisha mifumo na utaratibu wa masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kupanda mbegu kwa vijana ili kupata kizazi kilichobora ambacho kitasababisha nchi kuwa na wabunifu watakaokuja na bunifu zitakazokuza maendeleo ya taifa letu.

Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (DSTI), Profesa Ladslaus Mnyone alisema wizara iliandaa na kuridhia kwa uanzishwaji wa madawati ya majukwaa katika shule za msingi na sekondari ili kuhakikisha wanaendelea kuimarisha utaratibu na uhamasishaji wa masuala ya sayansi na ubunifu.

Mmoja wa mshiriki wa mafunzo hayo, Abubakar Hussein, alisema kuwa mafunzo haya yatawasaidia na watayafanyia kazi na kwa Mkoa wa Arusha watafanya vizuri kama maelekezo yalivyotolewa.

Mafunzo haya yanaendelea katika mikoa ya Tanga, Dar es Salaam na Arusha lengo likiwa ni kuimarisha mfumo wa uratibu na usimamizi wa masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu.





# Wenye ualbino waondolewa hofu kuhusu ukatili

**Na Vitus Audax**

SERIKALI imewatoa hofu watu wenye ualbino na kuahidi kuchukulia hatua katika kuwalinda, ikiwamo kuwafikisha katika vyombo vya dola watakaobainika kuwafanyia vitendo vya ukatili.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga alitoa kauli hiyo juzi baada ya kutokea tukio la kushambuliwa kwa mtoto mwenye ualbino Mei 4, mwaka huu katika Kijiji cha Mtakuja mkoani Geita.

Alisema serikali inakemea kitendo hicho kisichokua na utu na kuwaada wananchi kusaidia kudhibiti vitendo hivyo, kwa kuimarisha ulinzi ndani ya familia na jamii inayowazunguka.

Aidha, alizitaka kamati za ulinzi na usalama kuhakikisha vitendo vya aina hiyo vinadhibitiwa, akisema Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kushirikiana na Chama cha Watu wenye Ualbino Tanzania (TAS) kuelimisha jamii kuhusu haki za watu wenye ualbino.

Kadhalika, alitoa pole kwa familia ya mtoto Kazungu Malecha kwa kupatwa na mkasa huo, akisema tayari ofisi hiyo imefanya mawasiliano na Wizara ya Elimu kwa ajili ya mtoto huyo kusoma katika shule ya bweni.

Mwenyekiti TAS, Godson Mollel, alisema anaungana na wadau wengine wa haki za binadamu kupinga kitendo cha kikatili alichofanyiwa mtoto huyo.

Kaimu Mganga Mkuu Wilaya ya Geita, Dk. Stephen Mwaisombwa, alisema hali ya mtoto huyo inaendelea vizuri, anatarajiwa kuruhusiwa muda wowote.




Mkurugenzi wa Shirika la Women Ederly Advocacy and Development Organisation (WEADO), Eliasenya Nnko, akizungumza na Mabaraza ya Watoto Kata ya Lwabukande, wilayani Shinyanga juzi, katika kubainisha viashiria vya chanzo cha ukatili dhidi ya watoto huku akiwasihi kutoa taarifa za ukatili ili zipate kufanyiwa kazi. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Utitiri faini madereva bodaboda, bajaji kwamkera RC

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, amevionya vyombo vinashughulikia masuala ya usafirishaji wakiwamo askari wa usalama barabarani pamoja na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kuacha utitiri wa faini kwa waendesha bodaboda na bajaji.

Alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano na watoa huduma hao na kudai kuwa baadhi ya maofisa wamewageuza madereva bodaboda na bajaji kuwa kitega uchumi chao.

Alisema jambo hilo linachangia ongezeko la ajali, uvunjifu wa amani, kutokana na vijana hao kuvunja sheria kwa kutafuta fedha kwa nguvu ili kufidia fedha walizotoa.

Alisema serikali inatambua sekta hiyo binafsi kuwa ina vijana wengi waliojiajili, hivyo wanapofanya makosa waadhibiwe kwa mjibu wa sheria za nchi na siyo kuwafanya mitaji na kuleta usumbufu.

Katibu wa waendesha bodaboda, Abdulraazizi Bakari, aliiomba serikali kufanya maboresho ya miundombinu ya barabara ambayo imekuwa kikwazo katika shughuli zao, sambamba na kuomba kituo cha bodaboda katika eneo uwanja.

Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Mwanza, Sunday Ibrahim, aliwataka madereva bodaboda kuacha tabia ya kwenda kusoma vyuo mbavyo havijulikani kisheria ili kuepuka adha ya kutapeliwa fedha zao.

**Alisema jambo hilo linachangia ongezeko la ajali, uvunjifu wa amani, kutokana na vijana hao kuvunja sheria kwa kutafuta fedha kwa nguvu ili kufidia fedha walizotoa.**

## Lumbesa bado lawatesa wakulima wa mpunga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

LICHA ya serikali kupiga marufuku vipimo vya lumbesa bado, vitendo hivyo vinaendelea kufanyika hususani kwa wakulima waliopo vijijini.

Kilio hicho kimeibuliwa na wakulima wa mpunga Kata ya Lyamidati wilayani Shinyanga wakisema kuwa wafanyabiashara hao wamekuwa wakinunua mpunga kwa kutumia madumu makubwa na kuwasababishia hasara.

Akiwasilisha taarifa ya kata hiyo na kero zilizopo katika baraza la madiwani, Diwani Veronica Mabeja, alisema msimu wa kilimo mwaka 2023/24, wananchi wa kata hiyo wamepata mavuno mengi ya mpunga.

Alisema lakini wamejitokeza wafanyabiashara ambao wanafika katika mashamba ya wakulima na kulangua mazao yao kwa kutumia madumu makubwa.

Mwenyekiti wa Halmashauriya Wilaya ya Shinyanga, Ngassa Mboje, alisema suala hilo la wafanyabiashara kuwaonya wakulima limekuwa tatizo, kuahidi watalifuatilia ili kulidhibiti.

Alisema tabia hiyo imekuwa sugu na hivyo kuwafanya wakulima kushindwa kujikwamua kiuchumi kila msimu wa kilimo na kuendelea kuwa maskini kutokana na kupunjwa katika uuzaji wa mazao yao.

Baadhi ya wakulima wilayani Shinyanga walisema uuzaji huo wa mazao wa kupunjwa unatokana na kuhitaji pesa za haraka ili watimize mahitaji ya familia.

## RPC Mutafungwa ataka kuimarishwa ulinzi kila kata

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KAMANDA wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, amewaagiza wakaguzi kata mkoani hapa kusimamia kikamilifu ulinzi na usalama katika maeneo waliyopangiwa ili kukabiliana na vitendo vya uhalifu.

Alitoa agizo hilo juzi katika mkutano wa pamoja baina ya wakaguzi hao pamoja na watu wenye ualbino na viongozi wa ustawi wa jamii.

Mkutano huo ulilenga kuweka mipango ya pamoja katika kuimarisha ulinzi katika maeneo husika.

Kadhalika, aliwataka wakaguzi kata kwenda kuyatambua maeneo wanayoishi watu wenye ualbino, kusimamia mashauri yao mahakamani na kuangalia vitisho vya kiusalama pamoja na migogoro ya ardhi na familia.

Kamanda Mutafungwa aliwakumbusha watu wenye ualbino kuyapa uzito mambo ambayo siyo ya kawaida yanayojitokeza kwao, kwa kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Aidha, aliwaonya na kuahidi kuwachukulia hatua kali za kisheria waganga wa jadi ambao bado wanapiga ramli chonganishi.

Ofisa Ustawi wa Wilaya ya Nyamagana, Edith Ngowi, aliwataka wakaguzi kata kwenda kushirikisha kamati za watu wenye ulemavu zilizopo kwenye kata katika kutatua changamoto za makundi mbalimbali.

ALHAMISI MEI 16, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Mageuzi kuelekea nishati gesi asilia inavyoukaribishia umma afya bora**



Ukurasa 12

**Simulizi za watafiti; utumiaji bangi unavyombomolea ubongo mtumiaji**



Ukurasa 13

Mapinduzi Muhimbili, nusu wagonjwa wanaokolewa maisha huduma dharura

AFYA

## AKIPEWA MEZA KUONGOZA WATU...

# Kinachomng'arisha Samia kikaoni Ufaransa, unasaba wake na Mkataba Paris na vikao COP

**Na Mwandishi Wetu**

NAAM! Wasifu unaojitokeza, Tanzania inanguruma katika diplomasia uchumi duniani, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anaungana na vigogo wenzake duniani, akiwa mwalikwa wa Dk. Faith Birol, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Nishati Kimataifa ya Nishati, akawe Mwenyekiti Mwenza mkutanoni.


Wikiendi iliyopita akawasili jijini Paris, Ufaransa akapokea na wenyeji wakwe wanadiplomasia wa Kitanzania na wenzao wanaoishi huko.

Juzi, baada ya kupewa kipaza sauti mkutanoni jijini Paris, Mwenyekiti Mwenza, Dk. Samia akaorodhesha mambo manne, kuitetea Afrika katika uwanda wa nishati safi kimataifa.

Hapo anataja umuhimu wa kuwapo; ufadhili, suluhisho katika yanayohusu mazingira, hitaji la ushirikiano kimataifa na kushindwa kumudu gharama.

Wakati mama huyo wa Watanzania akishusha hoja zake katika mkutano wenye wajumbe 900, anazungukwa na wazito wengine jirani meza kuu hadi leo; Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guetress na kutoka shirika lake la afya (WHO), Dk. Thedros Adhanom Ghebreyesus na Mo Ibrahim, mwenye taasisi yenye jina hilo.

Siku chache kabla ya kuhudhuria kikao hicho anachohitimisha leo nchini Ufaransa, Rais Dk. Samia akazindua Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, lengo ni kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati hiyo ifikapo mwaka 2033.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa Ufaransa wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

Hapo akataka kuwapo nguvu ya pamoja kuanzia wahisani wa kimaendeleo, taasisi za umma na sekta binafsi kufanikisha azma hiyo.

Ni hatua inayokuja miezi michache baada ya kiongozi huyo kuongoza mkakati kwa nchi za Afrika, kuwawezesha kinamama wake kutumia nishati safi ya kupikia, aliposhiriki Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28), uliofanyika Dubai. Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Katika mkakati huo wa miaka 10, Rais Dk. Samia, anataka kuwapo nguvu za pamoja, kuanzia wahisani wa kimaendeleo, taasisi za umma na sekta binafsi ili kuongeza chachu kufikia malengo yake.

Hadi sasa kisera na kisheria, Tanzania ina mpango wa ushirikiano wa pamoja, kati ya sekta ya umma na serikali, uitwao PPP.

Mara ya mwisho, Rais Dk. Samia alikuwa jijini Paris, Februari 2022, akiuganisha hadi Ubelgiji kati ya Februari 9 na 19.

Nchini Ufaransa, akatia saini mikataba sita ya makubaliano, kwa nia ya kuendeleza uhusiano baina ya nchi hizo mbili, ikiwamo mkopo wa masharti nafuu kugharamia mradi wa ujenzi wa barabara wa mabasi yaendayo haraka, unaoendelea sasa.

Pia, akatia saini mkataba wa mkopo wa masharti nafuu, kuimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania kufikia malengo ya kutoa mikopo ya muda mfupi na mrefu kwa sekta ya kilimo.

Naye Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, akatia saini mikataba mingine ya ushirikiano kwa niaba ya serikali.

Pia, katika ziara hiyo akahutubia Shirikisho la Biashara la Ufaransa (MEDEF) mjini Paris, akifafanua serikali nchini inachukua hatua kuwerka mazingira muafaka ya kukuza sekta binafsi, akiwakaribisha wafanyabiashara wa Ufaransa kuwekeza Tanzania katika sekta kama za mifugo, Kilimo, Nishati, Madini. Pia, Rais Dk. Samia akakutana na Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron.

**MZIZI WA PARIS**

Hadi sasa, dunia inatekeleza Mkataba wa Paris wa Desemba mwaka 2015, ambao nchi 196 ziliingia makubaliano wakati huo, namna ya kusimamia mazingira ya dunia.

INAENDELEA UK.12

AFYA

# Simulizi za watafiti; utumiaji bangi unavyombomolea ubongo mtumiaji

Na Mwandishi Wetu



Uvutaji bangi ukiendelea. **PICHA: MTANDAO**

UNATAJWA mmea bangi umetumiwa na wanadamu kwa zaidi ya miaka 1,000, zaidi katika burudani; inavutwa au kumezwa.

Namna inavyoathiri akili za umma, inarejewa katika tafiti tatu zilizochapishwa na majarida yanayoitwa; Psychopharmacology na europsychopharmacology, pia International Journal of Neuropsychopharmacology, ikionyesha matumizi yake yanavyoathiri hatua za utambuzi na kisaikolojia.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Dawa na Uhalifu, liliripoti takriban milioni 192 duniani kote, kati ya umri miaka 15 na 64, wanatumia bangi kwa burudani, kurejea takwimu za mwaka 2018. Kuna makadirio asilimia 35 ya watumiaji, wana umri kati ya miaka 18 na 25, vijana ambao akili zao bado zinaendelea kukua.

Hivyo, matumizi hayo yanawagusa watumiaji waathirike zaidi katika ubongo, yanaopokuwa ya muda mrefu, kikiibua kinachoitwa 'Tetrahydrocannabinol.'

Kinachotajwa ni kiungo kikuu kinachoathiri ubongo katika bangi na eneo linaloathiri ni katika mfumo kunakoitwa 'endocannabinoid'; mahali penye mapokezi panapoguswa na kemikali tajwa.

Uwapo wa vipokezi hivyo unatajwa kuwa muhimu katika maeneo ya awali na ya viungo vya ubongo, vikidhibiti kemikali kwenye ubongo.

Maana yake ni kwamba kemikali 'dopamine' inahusika kuhisi, kujifunza, kutambua na kumbukumbu. Pia katika ubongo kunatajwa kuwapo kemikali zinazotajwa, ikiwamo kumbukumbu na kujifunza.

### ATHARI ZAKE

Utumiaji bangi unatajwa kuathiri mfumo wa utambuzi, tafiti zikisema wanaotumia kwa wingi wanangukia hatarini kuathirika. Hao ni watu wenye hamu ya kutumia kila mara na kuharibu shughuli zao za kila siku, kama vile kazi au kusoma.

Inakadiriwa asilimia 10 ya watumiaji bangi hukutana na tatizo la ugonjwa wa utambuzi na utafiti wa wasomo hao ulifanikiwa kuwapima takriban watu 39 wenye ugonjwa huo (waliachwa 'safi' katika siku ya upimaji) na kulinganisha na watu 20 wasiowahi kutumia bangi au mara chache.

"Tuliweza kuonyesha kwamba washiriki waliokuwa na tatizo hilo, walikuwa na utendaji mbaya zaidi wa kazi katika majaribio ya kumbukumbu ya Taasisi ya Cambridge Neuropsychological Test (jaribio lililoundwa kutathmini uwezo wa ubongo wa kuhifadhi kumbukumbu), ikilinganishwa na wengine ambao hawakuwahi au hutumia mara chache sana," inafafanua ripoti tajwa.

> **Kinachotajwa ni kiungo kikuu kinachoathiri ubongo katika bangi na eneo linaloathiri ni katika mfumo kunakoitwa 'endocannabinoid'; mahali penye mapokezi panapoguswa na kemikali tajwa.**

Utumiaji huo, pia umeonyeshwa athari mbaya katika 'utendaji wa kazi,' ambazo ni hatua za ubongo inayojumuisha fikra nyepesi na athari zinaonekana kuhusiana na umri wa matumizi ya dawa, huanzia kwa wenye umri mdogo, utendaji wao zaidi huathiriwa.

Pia mfumo wa utambuzi umegunduliwa kwa wasio watumiaji wa kila mara, kundi hilo kufanya uamuzi hatari zaidi kuliko wengine na lina matatizo zaidi ya kupanga.

Ingawa utafiti mwingi umefanyika kwa wanaume, kuna ushahidi tofauti ya athari katika jinsia tofauti, ingawa badi inabaki ukweli kwa wanaume wana kumbukumbu duni na ugumu wa kutambua vitu, huku wanawake wanaitumia bangi, wana matatizo ya umakini, pia katika utendaji kazi.

Ni tofauti zinazoendelea kutajwa, wakati tafiti zinafanywa kwa kuzingatia umri, upeo binafsi (IQ), matumizi ya pombe na nikotini, dalili za hisia na wasiwasi, utulivu wa kihisia na tabia.

### HISIA NA FIKRA

Matumizi ya bangi, pia huathiri hisia za watu, mfano baadhi ya utafiti wa awali unaonyesha hali ya kuhisi na kufikiri, pamoja na mizunguko ya ubongo inayohusika katika hatua hiyo, huathiriwa mtu anapotumia bangi.

Hilo linatajwa kuathiri utendaji shuleni au kazini, na linamfanya mtu ahisi kuwa na ari ya kazi na kutopata thawabu anapofanya vyema.

Katika utafiti wa wasomi hao, unatajwa walitumia kazi ya kufikirika, kwa washiriki walipitishwa kwenye 'skana' (mashine ya kuchunguza mwili) na kubaini athari kwenye mfumo wa hisia na athari za moja kwa moja za bangi kwenye mwili.

Washiriki utafiti hao walikuwa watumiaji wa wastani wa bangi na madhara yanajulikana zaidi kwa watumiaji wa muda mrefu. Pia kunatajwa kuwapo ushahidi, kwamba bangi inasababisha matatizo ya afya ya akili.

### MATATIZO KISAIKOLOJIA

Pia kukaonekana kila mara, wakati wa marufuku ya kutoka nje kutokana na janga la maradhi Covid-19, katika baadhi ya nchi, matumizi ya bangi kwa vijana yametajwa ni sababu ya kuendelea matukio kama hayo kisaikolojia.

Kuna utafiti unaoonyesha matumizi ya wastani ya bangi kuongeza hatari ya dalili za kisaikolojia kwa vijana, pia athari kubwa kwa walio na shida ya kisaikolojia.

Upo utafiti mwingine uliohusisha vijana 780, unapendekeza kwamba uhusiano kati ya matumizi ya bangi na uzoefu wa kisaikolojia unahusishwa na eneo la ubongo linaloitwa 'uncus'.

Hiyo inatajwa kuwapo ute unaoitwa 'par hippocampus' inayohusika katika kumbukumbu na kunusa, pia katika mchakato wa kusikia harufu, ikiwa na idadi kubwa ya vipokezi vyake 'cannabinoid.'

### BANGI YENYE NGUVU

Watafiti wanaeleza namna bangi yenye nguvu inavyoongeza hatari ya magonjwa ya akili, wanaotumia wakishindwa kuelewa mambo halisi, pia, wanashindwa kusikia hata sauti zao.

Utafiti unaeleza, bangi yenye nguvu yenye majani 'yenye miraba myeusi na myeupe ' inaongeza hatari ya mtu kupata magonjwa ya akili.

Inatajwa kwenye utafiti, inakadiriwa matukio ya kiakili yanahusishwa na bangi yenye nguvu, wakizingatia utafiti walioufanya kwenye miji ya barani Ulaya.

Jarida la Lancet, linataja bangi hizo kali zinauzwa zaidi katika miji ya London, Uingereza na Amsterdam, Uholanzi.

"Kama ukiamua kutumia bangi yenye nguvu ufahamu kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kuihatarisha akili yako," wanahitimisha watafiti hao.

### UVUTAJI KILA SIKU

Wataalamu hao wanabainisha utumiaji bangi ya kila siku, unachangia ongezeko la matatizo ya akili, Mtafiti Mkuu na mtaalamu wa magonjwa ya akili, Dk. Marta Di Forti, akifafanua: "Kama ukiamua kutumia bangi yenye nguvu ufahamu kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kuihatarisha akili yako."

Dk. Adrian James kutoka Chuo cha Royal Kitengo cha Magonjwa ya Akili, Uingereza anaitaja bangi yenye nguvu husababishia hali inayoitwa 'psychosis', kwa maana mtu kushindwa kutambua mambo, mtumiaji anasikia sauti, kuona visivyokuwapo, au mawazo mchanganyiko.

Matibabu yake yanatajwa kuwa tofauti na kawaida.

Hata hivyo, kuna tofauti za misimamo ya kitaifa, zikiwapo baadhi ya nchi zinahalalisha kisheria, matumizi hayo.

Madaktari nao wanahofia kuongezeka matumizi ya bangi yenye nguvu zaidi yenye kemikali aina iitwayo THC, inayowalewesha watumiaji.

Bangi yenye muundo wa cheche, ina kiwango cha juu cha THC asilimia 14 kwa sasa ina asilimia ndio imetawala katika mitaa ya London, Uingereza.

### BANGI IMENIHARIBIA

INAENDELEA UK.13

AFYA

# Mapinduzi Muhimbili, nusu wagonjwa wanaookolewa maisha huduma dharura

- Simulizi mtoto chupuchupu wiki tatu hajijui
- Huduma sasa zasambazwa ziwe za kitaifa

**Na Pilly Kigome**

KATIKA eneo moja la kiserikali kujivuna katika sekta ya afya, ni kwamba serikali inapiga katika kutekeleza miradi yake, ikitoa zao la wananchi wake wanapata huduma bora katika eneo hilo.

Sasa ni miaka 14 imepita, huko nyuma hapakuwapo baadhi ya huduma zinazoshuhudiwa sasa, utaalamu hadi miundombinu katika hospitali za kiserikali.

Taasisi ya Uhisani ya Abbort, kwa kupitia mfuko wake, kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania mwaka 2001, ziliingia ubia wa kuimarisha mfuko wa huduma za afya nchini, kwa kuwekezwa Dola za Marekani zaidi ya milioni 160, hapo inajumuisha elimu kwa wataaluma tajwa.

Mradi huo ulipofika mwaka 2010, ndipo ukaingia katika hatua ya kuainisha Idara ya Tiba ya Dharura katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, ambako madaktari bingwa wakapewa mafunzo ya tiba ya dharura katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Ni jitihada zilizozaa matokeo ya haraka kwa kupunguza vifo kwa asilimia 40 katika kipindi cha miaka miwili ya kwanza.

Miaka saba baadaye, 2017 kukatanuliwa huduma hiyo kwa kuanzishwa vituo vya tiba za dharura katika maeneo nane nchini, ikiwamo katika hospitali za rufani za mikoa ya Mbeya, Dodoma, Arusha,Tanga na Pwani.



Mkuu wa Idara ya Tiba za Dharura katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga-Bombo, Dk. Arafa Kachenje (kulia), akimhudumia Elly Amdason Kimodoa, mmoja wa wagonjwa walionufaika na huduma za dharura. Kushoto ni muuguzi katika hospitali hiyo, Scholastic Kideka Mundu. **PICHA: PILY**

### KUTOKA MUHIMBILI

Mkuu wa Idara ya Tiba ya Dharura Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. Juma Mfinanga, anasema tangu kuanzishwa kwa huduma hizo hospitalini hapo, sasa miaka 10, imeweza kupunguza vifo vitokanavyo na magonjwa ya dharura kwa asilimia 50, kutoka kuanzishwa huduma hizo mwaka 2010.

Anasema kwa sasa hospitalini hapo, vifo viko chini, wagonjwa wote wanaofikishwa katika huduma hizo na kuifanya Muhimbili kupiga hatua kubwa katika kutokomeza, au kuondoa changamoto ya kukabili vifo, ikilinganishwa na awali.

Anataja viwango vya vifo, vilikuwa juu kutokana na kutokuwa na changamoto ya kutokuwa na wauguzi na madaktari wabobezi katika kitengo hicho.

Dk. Mfinanga anafafanua siri kubwa ya mafanikio kutokomeza vifo hivyo ni kuongezeka kwa wataalamu kama wauguzi na madaktari wakipewa mafunzo ya kuhudumia wagonjwa hao kwa saa 24. Hiyo anaitaja inajumuisha kutobagua wagonjwa katika hali zao za kiuchumi, wadhifa na mwonekano binafsi, pindi wanapofikishwa hospitalini.

Hapo anafafanua kwamba. kitengo hicho kimewezesha kuondokana na janga la vifo na kwa sasa, kina uwezo wa kupokea wagonjwa 200 hadi 250 kwa siku kwa watu wazima na 50 hadi 70 kwa watoto. Anasema, wagonjwa wanaofikishwa katika kitengo hicho wana uhakika wa kupona kwa asilimia 99.5 ikilinganishwa na awali kabla ya huduma za dharura.

"Tunaomba kuwatoa hofu Watanzania kuwa wasiogope kukimbiza wagonjwa kuwafikisha hapa huduma za dharura ipo kwa ajili ya Watanzania wote wa hali zote bila kubagua.

"Wakifikishwa hapo mfumo ndio utasema mgonjwa yuko kwenye hali gani na kuanza kupatiwa huduma kwa haraka."

"Kuna aina tatu au madaraja matatu ya wagonjwa wapo wale wa alama nyekundu, kwa maana ya wagonjwa mahututi wasiojitambua," anasema Dk. Mfinanga na kufafanua:

### MAGONJWA DHARURA

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Magonjwa ya Dharura na Maafa Wizara ya Afya, Dk. Erasto Sylvanus, anasema serikali imejikita katika kuongeza huduma za dharura nchi nzima katika ngazi ya mkoa, wilaya, kata na vijiji ili kuendeleza kuboresha huduma za afya nchini kote.

Anaeleza kuna zaidi ya wataalamu 5,000 wakiwamo wauguzi na madaktari kutoka hospitali zingine, wameshafika Muhimbili kupatiwa mafunzo ya ubobezi wa magonjwa ya dharura katika chuo kinachotoa wataalamu hao kwa ushirikiano na udhamini kutoka Mfuko wa Abbott kutoka Marekani.

Huduma hiyo, anasema hadi sasa imeendelea kuokoa maisha ya Watanzania zaidi ya milioni 1.2 wameshapokea huduma za tiba za dharura kuanzia mwaka 2010 hadi sasa. Serikali kwa sasa inatekeleza upanuzi wa huduma hizo na kuanzisha idara mpya ya tiba hizo za dharura katika zaidi ya hospitali 100 nchini kwa ngazi ya wilaya na kata nchini.

Vyombo vya habari tayari vimeona juhudi hizo ngazi ya mikoa na kata kwa kutembelea Hospitali ya Mkoa wa Bombo Tanga kujionea juhudi kubwa zilizofanywa na serikali kwa ushirikiano na mfuko huo kuboresha huduma hizo katika maeneo tofauti ikiwamo miundombinu na kuanzisha huduma tiba ya dharura ikiwamo na kuwapelekea madaktari wabobezi.

Vilevile juhudi hizo hazikuishia hapo zilifika hadi ya kijijini kwa kutembelea Zahanati ya Kijiji cha Bantu, iliyopo wilayani Mkinga, kwa kuboresha na kupeleka huduma muhimu ya dharura, wagonjwa watibiwe na hapo na si kukimbizwa hospitali ngazi ya Taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Abbort Tanzania Prof. Hendry Sawe, anasema mfuko huo rafiki, unahudumia hospitali zote nchini hususani katika kuweka huduma wezeshi wa huduma za dharura.

Inaelezwa, mfuko huo umeshatoa msaada zaidi ya Dola za Marekani milioni 15 (Sh. 21,096,936,400) kuanzisha na kuendeleza tiba dharura nchini Tanzania, ikiwamo katika maeneo mengi muhimu, ikitoa huduma za afya na kufanya maboresho maeneo mengi katika hospitali nchini.

### USHUHUDA WA MGONJWA

Mmoja wa wagonjwa waliofanyiwa mahojiano na Nipashe katika Hospitali ya Taifa Muhimbili walioweza kuokoa maisha yao kupitia huduma hizo ni mtoto Dorica Cuthbert (8) mkazi wa Mpiji Majohe Mbezi jijini Dar es Salaam, aliyefikishwa hospitalini hapo mahututi.

Inatajwa ilikuwa, Mei 16, 2022 alipopata ajali ya kugongwa na bodaboda akiwa anatembea kando ya barabara, wakati anarudi nyumbani akitokea shuleni.

Alifikishwa hospitalini hapo akiwa hajitambui na kupokewa katika huduma hizo akabaki katikahali hiyo kwa wiki tatu, ndipo akaanza hata kupumua bila ya usaidizi wa mashine ya kupumulia.

Inatajwa hospitalini hapo Muhmbili, hali ya mtoto huyo imesharejea kawaida kwa asilimia 70; anaongea na kula, jambo ambalo awali lilikuwa kitendawili.

## Simulizi za watafiti; utumiaji bangi unavyombomolea ubongo mtumiaji

**INATOKA UK.12**

### BANGI IMENIHARIBIA

Ad Gridley, anayetumia aina tatu za dawa za dawa tiba ya akili, anasimulia kuugua ugonjwa unaoitwa 'chizophrenia' kumsababisha madhara, anashindwa kutambua au anatambua mambo kinyume na uhalisi, hata alishawahi kujaribu kujiua.

Anaamini maradhi hayo ya akili yalisababishwa na bangi, akaacha kuvuta. Anaendelea: "Nilikuwa ninavuta sana, ilikuwa kawaida kwangu kulewa na nilianza kwa kupewa kisha na kuanza kutumia mwenyewe.

'Baada ya kujaribu kujiua mara kadhaa, jambo ambalo sikulizungumzia, pia mama yangu aliniona nikiwa kwenye ghorofa nikining'iniza miguu yangu yangu, 'nikidensi', mara moja alijua kuna tatizo," anasimulia.

"Katika kipindi cha saa 24, daktari alipatikana na nikapelekwa hospitalini siku iliyofuata.

Imeharibu maisha yangu kwa miaka ipatayo 10 baadaye.

"Sikuweza kufanya lolote na nimekuwa nikilazwa hospitalini mara 10. Sikuwa ninafanya lolote la maana maishani mwangu.

"Nilipoacha kuvuta bangi, ugonjwa wa 'psychosis' ukaisha. Nilikuwa natumia madawa, kwa hiyo walau ubongo wangu ukaanza kuwa sawa.

Nilipoacha kuvuta, dalili za maradhi ya ubongo zikaanza kutoweka. Ningejua hatari za bangi sidhani kama ningeivuta."

- **Makala inatokana na andiko la mtaalamu wa afya ya akili, uharibifu wa mfumo wa 'neva' (mishipa), kutoka Kituo cha Utafiti cha Cambridge Biomedical Research Center (BRC); NIHR MedTech wakiwa na jopo la watafiti.**

MAZINGIRA

# Mageuzi kuelekea nishati gesi asilia inavyoukaribishia umma afya bora

**Na Joyce Lameck**

KUNATAJWA, kuna maendeleo katika mwongozo wa maendeleo endelevu na matumizi ya rasilimali ya gesi asilia na kuongeza faida zinazotokana na nishati hiyo.

Hiyo inarejewa inasaidia kuchangia kuleta mabadiliko na mseto wa uchumi wa Tanzania, pale mradi wa gesi kuziduliwa nchini, ni maendeleo pia fursa kwa wananchi mbalimbali katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Tanzania imekuwa ikifanya utafiti wa gesi asilia kwa zaidi ya miaka 50, ugunduzi wa kwanza wa gesi asilia nchini ulifanyika mwaka 1974 katika kisiwa cha Songosongo, kilichopo mkoani Lindi, kufuatiwa na ugunduzi wa pili katika eneo la Mnazi Bay mkoani Mtwara mwaka 1982.

Gesi asilia kutoka Songosongo iliuzwa kwa mara ya kwanza mwaka 2004 na ya kutoka Mnazi Bay mwaka 2006, ugunduzi huo umechochea kufanyika utafiti zaidi wa gesi asilia kwa maeneo ya nchi kavu na majini.

Kutoka na teknolojia kukuwa kwa kasi duniani, imeifanya Tanzania kuanza kutumia nishati ya gesi kwa ajili ya kupikia, ili kuacha kutumia njia za asili kama matumizi ya kuni na mkaa, ambayo yanasababiasha ukataji wa miti ovyo.

Pia, kunata madhara katika uchakataji wa mvua, kwani mazingira yaanaushawishi mkubwa katika kusaidia mvua kunyesha kwa kiwanda kitakachosaidia mazao kustawi vizuri na kuondokana na changamoto ya chakula nchini.

Vilevile, watu kuendelea kukata miti inasababisha misitu kupoteza mvuto na wakati mwingine misitu kufa kabisa kutokana na matumizi ya kuni na mkaa, kwani miti inakatwa na idadi inayopandwa ya miti ni ndogo na wakati mwingine huna miti inayopandwa kwa ajili ya kufidia.

Baada ya uchunguzi wa muda mrefu na kubaini changamoto hizo, serikali imekuwa ikifanya uhamasishaji kwa njia tofauti tofauti kwa wananchi ili waweze kutumia teknolojia katika matumizi ya gesi asilia ya kupikia.



Miundombinu ya kusambaza gesi asilia kutoka Mtwara inakochimbwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Kwa mujibu wa taarifa ya kiserikali, sasa kuna mkakati ambao maono yake ifikapo mwaka 2034, kada kubwa ya wananchi wawe na nishati safi ya kupikia ili kuondokana na matumizi ya nishati isio safi kwa kupikia na yenye athari kiafya kutokana na moshi.

Pia kwa makadirio ya wataalamu wa afya, takribani ya watu 33,000 kila mwaka, hupoteza maisha kutokana na magonjwa ya upumuaji yanayosababishwa na moshi wa kuni/mkaa wakati wa kupika, idadi kubwa ni wanawake kwani ndiyo huwajibika kwa shughuli ya kupika.

Hata hivyo wananchi tunapaswa kubariki kutoka kwenye utamaduni, ili kwenda kwenye teknolojia ili kutoka kule tulipo kwa kutumia nishati safi ya kupikia, si kubaki katika utamaduni unaosababisha kurudi nyuma kiuchumi.

Kutokana na utumiaji wa nishati ya gesi kwenye matumizi ya kupikia ni mwanzo wa kunufaika kwa kampuni na hata mtu binafsi katika uchakataji wa gesi hizo hadi kumfikia mtumiaji wa nishati hiyo kwani ni suala la ushirikiano na si kazi ya mtu mmoja.

Hivyo, gesi hiyuo inatengeneza na kutoa ajira za moja kwa moja kwa Watanzania, kundi kubwa linapata fursa za kibiashara kwa kampuni za wazawa zitatakazotoa bidhaa na huduma kwenye mradi katika kipindi cha uendelezaji.

Ukuaji wa viwanda uendelezaji wa shughuli za utafutaji na uzalishaji wa gesi ya kina kirefu baharini, nao ni fursa ya uzalishaji gesi nyingi zaidi, itakayoweza kutumika nchini na kuongeza fursa kwa watu ambao tayari wameshajikita kwenye uzalishaji na usambazaji wa gesi.

Ongezeko la mapato serikali itajizalishia mapato makubwa kila mwaka na hivyo kusaidia wananchi wa Tanzania katika shughuli za kupika nchini, pia kuepukana na maradhi yatokanayo na moshi wa kuni na mkaa.

Kwa Watanzania sasa ni muda wa kwenda na tekinolojia hii ili kuendelea kunufaika na nishati safi ya kupikia, uacha dhana za za kitamaduni ambazo zimekuwa zikileta matokeo hasi kwa jitihada za serikali katika kupeleka mahali sahihi kutokana na teknolojia kukua duniani.

## Kinachomng'arisha Samia kikaoni Ufaransa, unasaba wake na mkataba

**INATOKA UK.11**

Katika utekelezaji wake, Rais Dk. Samia na Tanzania kwa jumla inaonekana kuwa mdau mkubwa na mwenye heshima kubwa. Kurejea lugha ya watafiti, simulizi za mizizi wa jambo zinazobeba ukweli wa jambo ulipo.

Mnamo Juni 2014, Samia akiwa Waziri wa Nchi mwenye dhamana na Mazingira, Tanzania ilihudhuria kikao cha Umoja wa Afrika (AU), jijini Malabo, Guinea ya Equator, Rais Jakaya Kikwete, akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya AU.

Ni wakati huo, Umoja wa Mataifa ukisaka kuridhiwa hoja ya makubaliano ya Paris. Aliyekuwa Katibu Mkuu, Ban Ki-moon (2007 - 2016), raia wa Korea, akatumia kampeni kwa baadhi ya wadau zake wakati huo, akiwamo Jakaya Kikwete, marafiki tangu wote wakiwa mawaziri wa Mambo ya Nje.

Ban Ki Moon, akatua kikaoni Malabo na kuwashawishi wana AU, kutenda na kufanikisha. Ni katika hatua hizo zote, mkono wa kufanikisha mikakati yake, ni Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais wakati huo, Samia.

Miezi mitatu baadaye, ushawishi wa Ban Ki- moon, ulikuwa umegusa bara zote za duniani Septemba, 2014, nchi za dunia zilikusanyika Washington Marekani, kwa maridhiano ya awali kuhusu makubaliano ya Paris.

Mwaka uliofuata 2015, Rais Kikwete akiwa amestaafu miezi miwili na Rais Dk. Samia, akiwa Makamu wa Rais, ofisi yake ikiwajibika moja kwa moja na Muungano na Mazingira, kukashuhudiwa, mwezi Desemba Mkataba wa Paris unaafikiwa.

Baada ya kupitishwa Mkataba wa Paris, ndio chombo hicho cha kusimamia mazingira duniani, kikabuni mikutano inayoitwa 'COP' inayohama kati ya nchi moja na nyingine, kutafakari, kubuni na kutekeleza maudhui ya Mkataba wa Paris.

Kimsingi, ndio hata inayoanika unasahaba wa Rais Dk. Samia na masuala ya mazingira nchini na kimataaifa, Mkataba wa Paris na mikutano ya COP, kama iliyofanyika Dubai mwaka jana.



## Serikali yapata mwarobaini wa “tuma kwenye namba hii”

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye amesema uhalifu wa mitandaoni umeendelea kupungua kutokana na mikakati inayofanywa na serikali, ikiwamo kuanzisha mfumo wa namba maalum ya kupokea na kuzifungia laini zinazobainika kufanya utapeli.

Nape aliyasema hayo bungeni jana alipojibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Buhigwe (CCM), Kavenjuru Felix. Mbunge huyo alitaka kauli ya serikali kutokana na wizi wa mtandaoni kuendelea na sababu za kutokamatwa wahalifu hao ilhali laini zinasajiliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na polisi wanaruhusiwa kuchukua taarifa zozote za laini zilizosajiliwa.

Akijibu maswali hayo, Waziri Nape alisema kazi ya TCRA si kukamata wahalifu bali kuwezesha polisi kupata ushahidi wa kuwapata wahalifu.

Alisema TCRA ina jukumu la kufungia laini na kwa Septemba 2023 kulikuwa na laini za uhalifu 23,328 na zilipungua hadi kufikia 21,000 mwezi Desemba mwaka huo.

Alisema kuwa hadi Machi 2024 kulikuwa na laini za simu 17,318 huku akidai walipoanza uhakiki kulikuwa na laini milioni 9.045 ambazo hazijahakikiwa na walifungia laini 907,046.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali kukomesha wizi wa mtandaoni; naye Waziri Nape akijibu swali hilo, alisema serikali tayari imechukua hatua kadhaa kwa ajili ya kuweka mazingira salama kwa wananchi hususan kwenye mitandao.

“Mwaka 2015, serikali ilitunga Sheria ya Makosa ya Mitandao na Sheria ya Miamala ya Kielektroniki kwa lengo la kutambua miamala inayofanyika kimtandao, pia kutambua kisheria makosa yanayofanyika kwenye mitandao ili kuchukua hatua stahiki yanapobainika makosa hayo,” alisema.

Pia alisema katika kujenga mazingira salama ya kisheria, serikali imetunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022 ambayo lengo kuu ni kuweka utaratibu wa kuhakikisha wakusanyaji taarifa wote wanafuata misingi ya kulinda taarifa za mwananchi.

Alisema serikali ilianzisha Kitengo cha Uhalifu wa Mitandao chini ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa makosa ya mitandao ikiwamo wizi wa aina yoyote kwenye mtandao na kuandaa majalada ya kufungulia mashtaka kwa kusaidiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

“Serikali kwa kushirikiana na Watoahuduma wa Simu za mkononi imeanzisha mfumo kupitia namba ‘15040’ wa kupokea na kuzifungia namba ambazo zimeripotiwa na kuthibitika kutuma ujumbe au kupiga simu za utapeli.

“Baada ya kuthibitisha namba hizo kufanya vitendo hivyo, namba husika hufungiwa, kitambulisho cha NIDA kilichotumiwa kusajili namba husika kufungiwa kusajili na kifaa kilichotumika (simu) pia kufungiwa ili kisifanye kazi,” alisema.

# TCDD walia na kukua Deni la Taifa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTANDAO wa Madeni na Maendeleo Tanzania (TCDD) umesema kukua kwa Deni la Taifa kila mwaka kunasababisha baadhi ya wizara kukosa bajeti ya kutosha kutekeleza miradi ya maendeleo, kikiishauri serikali “kukopa kwa uwajibikaji”.

Mkurugenzi Mtendaji wa TCDD, Hebron Mwakagenda, aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati wa kikao kazi cha kujadili mwenendo wa Deni la Taifa.

Alisema kuwa kutokana na mwenendo wa deni hilo ulivyo hivi sasa, serikali inapaswa kukopa kwa uwajibikaji ili mikopo ielekezwe kwenye miradi iliyokusudiwa na si vinginevyo.

“Serikali inapaswa kukopa kwa uwajibikaji ili kiasi chote kiende kule ambako kinahitajika na si kufanya mambo mengine, pia ikope pale tu panapokuwa na uhitaji au kama inaona huo mradi hatuwezi kufanya kwa fedha zetu za ndani. Ni muhimu pia iangalie maslahi ya kizazi kinacho,” alisisitiza.

Mwakagenda alisema kukua kwa Deni la Taifa kuna athari kubwa kwa nchi kwa kuwa serikali imekuwa ikitenga kiasi kikubwa cha fedha kwenye bajeti yake ya kila mwaka hudumia deni hilo.

“Deni la Taifa lina athari kubwa sana kwa taifa letu. Kwa mfano, katika bajeti ya mwaka huu (2023/24), serikali imetenga Sh. trilioni 10 kwa ajili ya kuhudumia deni la taifa, kiasi ambacho ni kikubwa kuliko hata bajeti ya baadhi ya wizara,” alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa kutokana na hali hiyo, Bunge linapaswa kusimamia wenye dhamana kukopa kwa tija na fedha hizo kuelekezwa kwenye mambo yaliyokusudiwa.

“Wananchi lazima kupiga kelele kuhusu kukua kwa Deni la Taifa, watu wengi wanaona kama deni haliwahusu, lakini ukweli ni kwamba deni hili lina athari kubwa sana kwetu, hivyo lazima Bunge lisimamie wahusika ikiwamo Wizara ya Fedha ambao ndiyo wakopaji, wakope pale tu kwenye ulazima na si vinginevyo,” alisema.

Ofisa Miradi wa TCDD, Boniface Komba, alisema kukopa si tatizo bali kinachotakiwa ni kuhakikisha fedha zinazokopwa zinaelekezwa kwenye miradi na si vinginevyo.

“Kukopa si vibaya lakini wahusika wanapaswa kusimamia fedha hizo ziende kwenye miradi iliyokusudiwa. Kama ni ujenzi wa SGR (reli ya kisasa), basi ziende huko, si sehemu nyingine,” alifafanua.

Alisema jamii pia inapaswa kutunza miradi ambayo imetumia kiasi kikubwa cha fedha ili iwe na tija kwa taifa.



Waziri wa Fedha, Dk Mwigulu Nchemba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na ujumbe kutoka Benki ya Maendeleo TIB ulioongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki, Sosthenes Kewe baada ya mazungumzo yao, jijini Dodoma juzi. Walijadili kuhusu namna benki hiyo inavyoweza kuwezesha shughuli za uwekezaji ili kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake na nafasi ya Wizara ya Fedha katika kuhakikisha benki ya TIB inatimiza malengo ya kuanzishwa kwake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aonya vijana kelele mitandaoni

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego amewataka vijana kujitambua na kufanya kazi kwa bidii badala ya kupiga kelele kwenye mitandao ya kijamii.

Alielekeza hayo jana wakati wa maadhimisho ya miaka 35 ya huduma ya Hospitali ya Rufani ya Mtakatifu Gaspar iliyoko Halmashauri ya Itigi, wilayani Manyoni. Hospitali hiyo inamilikiwa na Kanisa Katoliki.

“Niwaombe vijana wa Itigi, Manyoni, Singida na Tanzania kwa ujumla wafike hapa St. Gaspar waone jinsi wenzao wanavyochapa kazi. Vijana si kelele kwenye mitandao, vijani ni kujitambua na kufanya kazi ambayo jamii inaiona kwa macho,” alisema.

Dendego alisema katika kukagua hospitali hiyo, amefurahishwa na jinsi uwekezaji mkubwa wa vifaa ulivyofanyika na kikubwa zaidi ni jinsi mazingira ya hospitali hiyo yalivyo mazuri na yanavyovutia.

Alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa Taasisi ya Mtakatifu Gaspar ili iendelee kutoa huduma bora zaidi na kwamba ndoto kubwa aliyonayo Rais Samia Suluhu Hassan ni kupambana na vifo vya wajawazito na watoto.

Mkuu wa Mkoa alisema serikali imejenga vituo vingi vya afya na zahanati ili kusogeza huduma karibu kwa wananchi na katika kufanikisha utoaji huduma za afya, ni lazima kushirikiana na taasisi binafsi.

“Tunawashukuru, tunawaheshimu na kuwathamini sana wamisionari wanaotuunga mkono, nikuombe mkurugenzi kama kuna changamoto zozote mnazozikabili nikabidhini nizitafutie ufumbuzi na nimefurahishwa kila nilipopita kukagua nimekuta wanaohudumia ni vijana,” alisema Dendego.

Mkurugenzi wa Hospitali na Chuo cha Mtakatifu Gaspar, Padre Justin Boniface, alisema Taasisi ya Mtakatifu Gaspar imepata mafanikio makubwa tangu kuanzishwa kwake mwaka 1987, ushirikiano mkubwa kutoka serikalini ukiwa sehemu ya chachu ya mafanikio hayo.

Alisema katika maadhimisho haya mwaka huu taasisi imeboresha huduma zaidi kwa kukarabati wodi ya wanawake na kuwekewa vifa vifya vya kisasa ili kuwezesha kinamama kupata huduma bora.

Padre Boniface alisema mwaka huu hospitali imeanza kujenga kitengo cha kusafisha damu ambacho kwa Mkoa wa Singida huduma hiyo inatolewa na taasisi moja.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemirembe Lwota, alipongeza wafanyakazi kwa kazi nzuri wanazofanya na kuwataka waendelee kufanya kazi kwa bidii ili sifa zilizopo katika taasisi hiyo zifike zipae kimataifa.

Hospitali ya Rufani ya Mtakatifu Gaspar ilianza kama zahanati mwaka 1987. Miaka miwili baadaye ilizinduliwa rasmi kuwa hadhi ya hospitali ya ngazi ya wilaya na Rais Ali Hassan Mwinyi.





# Hatimiliki 700 kutolewa kwa wananchi Suma, Nditu

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

ZAIDI ya hatimiliki 700 zinatarajiwa kutolewa kwa wananchi wa vijiji vya Suma na Nditu vilivyoko katika Kata ya Suma Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya baada ya upimaji wa maeneo ya wananchi kukamilika na kupunguza migogoro ya ardhi.

Upimaji huo wa maeneo ya wananchi unafanywa na Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi na mradi huo kwa Wilaya ya Rungwe unatekelezwa katika vijiji viwili pekee.

Ofisa Srdhi kutoka Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi ya ardhi, Boniface Magige, alisema mpaka sasa katika kijiji cha Nditu wameandaa hatimiliki 473 na kijiji cha Suma hati 266 kwa ajili ya kutolewa kwa wananchi.

Alisema utaratibu huo unakwenda sambamba na utoaji wa elimu kuhusu matumizi bora ya ardhi kwa wananchi wa maeneo hayo ili kuwajengea uwezo wa kusimamia na kutumia ardhi kwa kuzingatia mpango wa matumizi iliyowekwa.

"Kazi hii imeshakamilika na tayari wananchi wamepata fursa ya kuja kuhakiki na kusaini hati zao kwa ajili ya hatua zinazofuata ili kukabidhiwa hati zao, kwa sasa tunasubiri hatua za mwisho ili wakabidhiwe," alisema Magige.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nditu, Austine Lupogo, aliishukuru serikali kwa hatua ya kupima na kuwamilikisha wananchi wake maeneo kisheria hatua itakayosaidia kupunguza migogoro ya ardhi kijijini hapo.

Alisema awali wananchi hawakuelewa mpango huo wakidhani una lengo la kuchukua maeneo yao, lakini baada ya Tume ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kutoa elimu wamepata uelewa na wamefurahia hatua hiyo.

Mmoja wa wananchi wa kijiji cha nditu, Agnes Sikwese, alisema mpango huo una manufaa kwa sasa na kwa vizazi vya baadaye kwa kuwa wamepata hatimiliki ambazo zinawapa uhalali wa kumiliki maeneo yao.

Aidha, alisema kupata hatimiliki kutawasaidia kupata fursa mbalimbali ikiwamo mikopo huku akishauri mpango huo kuwa endelevu kwa wananchi wa vijiji vingine ili waweze kunufaika kama wao walivyonufaika.




Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akipiga kengele kuashiria kuorodheshwa rasmi kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) katika Soko la Hisa Dar es Salaam, wakati wa hafla iliyofanyika ofisi za Hazina, jijini Dodoma jana, huku wageni wengine wakishuhudia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TRA kuimarisha mipaka Tanzania, Zambia kiufanisi

**Na Renatha Msungu**

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zambia (ZRA), Dingani Banda wameweka mikakati ya kuimarisha utendaji kazi wa mpaka wa Tanzania na Zambia, Tunduma ili kuwahudumia kwa ufanisi wasafiri na wasafirishaji kutoka pande zote.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamishna Kidata alisema wamejipanga kuimarisha mpaka wa kuingia Tanzania na kwenda Zambia.

Alisema wataalamu kutoka Tanzania na Zambia wako imara katika utendaji kazi zao za kila siku kwa wafanya biashara na jamii.

"Tumekubaliana kwa pamoja kuimarisha utendaji kazi wa mpaka huu kwa sababu ni muhimu kwa maslahi ya nchi zetu na tunaimarisha mifumo ya forodha, ufanisi na uwajibikaji katika kurahisisha mifumo ya uvushaji mizigo na bidhaa na kuzuia mianya yote ya magendo," alisema Kidata.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zambia (ZRA), Dingani Banda, amepongeza ujio wa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, ambaye aliongozana na timu ya viongozi mbalimbali kutoka TRA na kuahidi kuwa yeye na timu yake watayafanyia kazi maazimio mbalimbali waliyokubaliana katika mkutano huo na kupanga tena siku nyingine ya kukutana na kupeana mrejesho.

Aidha, makamishna hao wamejadili na kukubaliana kuimarisha mikakati ya pamoja ya kuboresha mpaka wa Kasesya uliopo wilayani Kalambo mkoani Rukwa ambao utapunguza msongamano wa magari katika mpaka wa Tunduma.

"Tumekubaliana kuimarisha mpaka wa Kasesya ambao kwetu ni wa kimkakati na nimepita jana kujionea mwenyewe hali ilivyo pale kwa sababu ni fursa kwetu," aliongeza Kidata.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa Ofisa Mfawidhi wa Forodha wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kassim Mhando, makusanyo ya kodi mpakani hapo katika kipindi cha miezi 10 yaani kuanzia mwezi wa Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 TRA TRA ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 122.3 kati ya lengo la kukusanya Sh. bilioni 120.5 sawa na ufanisi wa asilimia 101.5.

Pia, aliongeza kuwa moja ya manufaa ambayo nchi ya Tanzania na Zambia inanufaika na mpaka huo wa Tunduma ni wastani wa uvushaji magari kwa siku ambao ni zaidi ya magari elfu moja yanayotoka kuingia Tanzania na hiyo imetokana na matumizi thabiti ya skana mpya ya kisasa inayoweza kuvusha magari mengi kwa muda mfupi na kuepusha foleni.

"Moja ya faida zinazopatikana katika mpaka huu ni idadi ya mizigo inayoenda nje ya nchi inaongezeka mwaka hadi mwaka hali ambayo inapelekea mapato kuongezeka," alisema Mhando.

Alisema hali ya udhibiti wa magendo mpakani hapo kupitia Idara ya Forodha katika Kitengo cha Udhibiti na Ushurutishaji imekua nzuri kwa sababu kitengo hicho kinafanya doria mbalimbali na kimekua kikikamata magendo, kwa mfano kwa mwaka huu wa fedha kimekamata jumla ya tani 160 za vipodozi ambavyo vimethibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuwa havifai kwa matumizi ya binadamu.

Makamishna wote wawili wamekubaliana kwa pamoja kukutana tena mapema mwezi Agosti mwaka huu kwa ajili ya mrejesho wa mambo waliyokubaliana katika kikao walichofanya mjini Tunduma.

# RC aonya wanaofanya shughuli vyanzo vya maji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amewaonya wananchi wa kijiji cha Mavanga wilayani Ludewa mkoani humo kutofanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji ikiwamo kuingiza mifugo.

Alitoa kauli hiyo katika ziara ya siku tatu ya kutembelea miradi wilayani Ludewa na akiwa Kijiji cha Mavanga, wananchi walilalamikia uchafu wa maji ya bomba kwenye mradi unatekelezwa kijijini hapo wenye thamani ya zaidi ya bilioni 1.3 utakaohudumia wakazi wapatao 5,000.

"Ni kweli dinga zipo, lakini maji yanachafuliwa na shughuli za kibinadamu, mtashikana uchawi bure lakini wachawi ni sisi wenyewe, Rais ameshatimiza wajibu wake fedha zimefika, wekundu wa maji unasababishwa na ng'ombe," alisema Mtaka.

Alitoa wito kwa viongozi wa kijiji na kata kushirikiana katika kujiwekea sheria ndogo ndogo kwa ajili ya kulinda vyanzo vya maji.

"Kwenye WADC wekeni sheria, mkitaka mtusaidie watu wenye ng'ombe kwenye eneo la chanzo watoe ng'ombe, watu wanaolima kule karibu na chanzo watoke, kwa sababu kuna siku mradi utakamilika maji yatakuwa hayatoki chanzo kitakuwa kimekauka," alisisitiza.

Aidha, alimpongeza mkandarasi mzawa anayetekeleza mradi huo Emirate Builders Co. Ltd kwa kuonesha uzalendo kwa kutumia mtaji wake ili kukamilisha mradi huo.

"Tunahitaji makandarasi kama Emirate ametekeleza mradi mpaka hatua hii kwa malipo ya asilimia 15, tungekuja hapa tukute mawe mashimo na picha nzuri ya tengi la maji, lakini ametumia fedha ya mtaji wake, lakini pia amekubali maboresho ya nyongeza, mnapopata miradi mingine watu wa hivi wapeni," alisema Mtaka.

Awali, mmoja wa wananchi wa kijiji hicho Musa Mwabena, aliishukuru serikali kwa mradi huo, lakini alilalamikia changamoto ya maji ya bomba kutoka yakiwa machafu hali ambayo inahatarisha afya zao.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Wilaya ya Ludewa, Mwita Isaya, alisema utekelezaji wa mradi huo wa kijiji cha Mavanga unalenga kuimarisha miundombinu ya mradi wa awali kwa kujenga miundombinu mipya, kupanua mtandao wa maji na kuongeza huduma ya maji kutoka kwenye chanzo kipya cha mto Msolwa.

Naye mhandisi wa mradi huo, Ombeni Mwanri, kutoka kampuni ya Emirate Builders Co Ltd alisema mradi huo umefikia asilimia 97 na kuahidi kufanyia kazi maagizo yaliyotolewa ikiwamo ujenzi wa chujio na ngazi za kupunguza uchafu pamoja na kuhakikisha maji yanatoka katika vituo viwili vilivyopo jirani na tangi la maji.

Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi Mkoa wa Njombe Josaya Luoga, alitoa rai kwa wananchi kuondoa mifugo katika eneo la chanzo na kuweka uzio kukilinda.





## CAG abaini utoaji mikopo haukuzingatia sheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, Dk. Othaman Abassi Ali, amesema katika ukaguzi wake kwa mwaka wa fedha 2023 katika Benki ya Serikali ya Watu wa Zanzibar (PBZ), amebaini kasoro za kutozingatiwa kwa matakwa ya kisheria katika utoaji wa mikopo.

Akiwasilisha ripoti yake mbele ya Rais wa Zanzibar hivi karibuni, katika viwanja vya Ikulu visiwani humo, alisema mikopo hiyo ilikuwa na thamani ya Sh. bilioni 1.04 ambayo walipewa wafanyakazi wake sita bila ya kuzingatia miongozo na sera za utoaji wa mikopo ya benki.

Alisema ukaguzi wake umebaini wakati wa utoaji wa mikopo hiyo waliopatiwa walikuwa hawajathibitishwa kazini kinyume na toleo la utumishi wa umma la Febuari 21, 2022.

Alisema dosari nyingine ni mkopo huo haukupata idhini ya bodi ya wakurugenzi wa benki hiyo jambo lililosababisha kukosekana kwa uhalali wa uidhinishwaji wa mikopo hiyo.

Alisema mikopo hiyo iliyotolewa haiendani na muda wa mkataba wa ajira za wanufaika hao na ajira za mkataba zilikuwa na ukomo wa miaka mitatu, lakini waliopatiwa wanufaika hao ilikuwa na ukomo wa urejeshwaji baina ya miaka mitano hadi saba kinyume na sera ya mikopo ya benki.

Alisema kwa mujibu wa sera ya mikopo ya mwaka 2023, iliweka ukomo ya kiwango cha uidhinishwaji wa mikopo kwa watumishi kwa kiwango cha thamani ya mkopo chenye thamani ya shilingi milioni 200 ambao utaidhinishwa na mkurugenzi mtendaji wa PBZ na endapo kiwango hicho kitazidi kwa mtumishi wa PBZ italazimika kuombwa ridhaa kwa bodi ya benki hiyo.

Alisema cha kustaabisha kwamba uongozi wa benki hiyo ulitoa mikopo kwa watumishi wawili yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 200 kwa kila mtumishi mmoja bila ya kushirikishwa bodi wa wakurugenzi wa PBZ jambo ambalo ni kinyume na sera ya mikopo waliojiwekea.

Akizungumzia uwanja wa michezo Gombani Pemba, Dk Abbasi alisema katika ukaguzi wake umebaini kuwepo kwa dosari ya usimamizi duni wa mradi wa usimamizi wa mkataba, kukosekana kwa udhibiti wa ubora, kutofuatwa kwa sheria na kanuni na ununuzi.

Alisema pia dosari nyingine ni mipango duni na usanifu wa mradi na kutopekuliwa kwa rasimu ya mkataba na mwanasheria mkuu wa serikali kwa lengo la kutolewa maoni ya kisheria kwa mujibu wa sheria namba 11 ya ununuzi na uondoshaji wa mali ya umma ya mwaka 2016.

Hata hivyo, alisema katika kipengele cha usimamizi wa kifedha ukaguzi wake ulifanya tathmini juu ya uwepo wa ufanisi katika utoaji wa fedha zilizopangwa na kuidhinishwa kwa matumizi ya mradi, ufanisi wa udhibiti wa ndani wa kifedha na kuzingatia kanuni za kifedha zinazoongozwa na hali ya malipo kama ilivyooneshwa katika hati za mradi husika.

"Licha ya mradi huo kupangiwa jumla ya shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya ukarabati kumebainika kujitokeza kwa ongezeko la gharama za ziada ya shilingi bilioni 2.842 na kusababisha ukarabati huo kufikia shilingi bilioni 5.642 sawa na ongezeko la asilimia 101.5 jambo ambalo ni kinyume na sheria namba 11 ya ununuzi wa mali za umma ya mwaka 2016," alisema.

Aidha, alisema pamoja na dosari hiyo, lakini pia ukaguzi wake umebaini kupewa kazi ya mkataba kwa mkandarasi ambaye hakuwa na sifa na vigezo na kanuni namba 85 kanuni ndogo ya tano ya kanuni ya manunuzi ya umma ya mwaka 2020 inaeleza kwamba taasisi ya ununuzi na uondoaji wa dhabuni itathmini sifa ya zabuni kwa mujibu wa vigezo na taratibu za kufuzu zikiwamo katika nyaraka za kabla ya kufuzu ikiwa zipo na katika nyaraka za zabuni au nyinginezo za kufanya zabuni au nukuu.

"Ukaguzi wangu ulifanya mapitio ya barua kutoka mamlaka ya ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya tarehe 14 Machi 2020 kuhusu mapendekezo ya zabuni," alisema.



Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Jacobs Mwambegele (katikati), akizungumza na waandishi wa habari Mjini Unguja, Zanzibar jana, kuhusu uzinduzi wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura unaotarajiwa kufanyika Julai 01 mwaka huu. Kulia ni Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume, Ramadhan Kailima na Makamu Mwenyekiti wa Tume, Jaji Mstaafu Mbarouk Salim Mbarouk. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi asema utalii kichocheo uchumi usafiri wa anga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, amesema utalii ni muhimu kwa mikakati ya maendeleo ya uchumi wa nchi na usafiri wa anga ndio kichocheo kikuu cha ukuaji wa uchumi huo.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kongamano la kimataifa la masuala ya anga la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika visiwani Zanzibar na kuwashirikisha washiriki zaidi ya 200 kutoka nchi mbalimbali ikiwamo Uganda, Afrika Kusini, Sudan, Burundi, Somalia, Ethiopia na Kenya.

Dk. Mwinyi alisema, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazingatia mikataba yote ya usafiri wa anga ya kimataifa ili kuhakikisha ukuaji wa sekta hiyo unaendelea kuwa salama.

"Nchi yetu inajivunia mafanikio ambayo yamefikiwa katika sekta ya usafiri wa anga. Nachukua fursa hii kuwataka wadau na washirika wa usafiri wa anga kuimarisha ushirikiano ili kuhakikisha sekta hiyo inaendelea kukua kwa usalama," alisema.

Alitaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kuwa Tanzania imeendelea kushirikiana na nchi washirika chini ya mwavuli wa Taasisi ya udhibiti wa usalama wa usafiri wa Anga ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika kuoanisha kanuni za usafiri wa anga ndani ya ukanda huo kwa lengo la kuwianisha taratibu, kuimarisha usalama na kuongeza ufanisi.

Alisema pia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupata asilimia 87 ya usalama na ufanisi, mpango wa kimataifa wa ukaguzi wa usalama wa kimataifa uliofanywa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) mwaka jana, ni kukuza usalama wa usafiri wa anga duniani kupitia ukaguzi na ufuatiliaji wa mara kwa mara wa nchi wanachama.

Aidha alisema mafanikio mengine ni uboreshaji wa mradi wa masafa ya mbali (VHF) unaojumuisha pia ufungaji wa vituo 18 vipya na redio katika viwanja vya ndege 12, na uwekaji wa mifumo ya kinasa sauti katika viwanja vinne vya ndege.

"Uwekaji wa mfumo wa Kutua kwa Ndege (ILS) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume ni ushahidi wa wazi kuhusu nia yetu ya kufanya usafiri wa anga kuwa salama na hivyo kuwa mwezeshaji wa sekta ya utalii ambayo, kama nilivyosema awali, ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu," alisema Dk. Mwinyi.

Aliwataka washiriki wa kongamano hilo kujadili na kutoa mapendekezo sio tu jinsi changamoto zilizoainishwa katika maeneo hayo zinavyoweza kutatuliwa, bali pia kubainisha jinsi fursa zinazohusiana na maeneo hayo zinavyoweza kutumika kikamilifu kwa manufaa ya usalama wa anga, uwezo, ufanisi na ulinzi wa mazingira katika Ukanda wa nchi zetu za Afrika Mashariki.

**Dk. Mwinyi alisema, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazingatia mikataba yote ya usafiri wa anga ya kimataifa ili kuhakikisha ukuaji wa sekta hiyo unaendelea kuwa salama.**

Alizishukuru nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Bodi ya Taasisi ya Udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC CASSOA) kwa kuipa nafasi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuandaa kongamano hilo.

Alisema moja ya malengo ya CASSOA ni kusaidia nchi wanachama katika kutimiza majukumu yao ya udhibiti wa usalama chini ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkataba wa Chicago.

Pia, alisema nchi inaendelea kunufaika na uhusiano mzuri wa kufanya kazi na nchi zote Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaozingatia dira ya pamoja na uelewa wa kina kwa madhumuni ya usalama wa anga na kwa maendeleo ya Mataifa hayo.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohammed, alisema watu wengi wanafikiria usafiri wa anga ni salama na haraka hivyo ni muhimu wadau wakawa na uwelewa wa kutosha juu ya mada ya usalama ambayo itazungumziwa katika kongamano hilo.

Alisema suala la usalama sio la kupuuziwa na abiria wanaosafiri matarajio yao ni kufika salama na wanapopata msukosuko abiria huingia na taharuki.

Spika wa Bunge la Afrika Mashariki, Joseph Ntakiruimana na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki masuala ya anga, Hamza Johari, walisema wameanzisha jumuiya ya anga ili kusaidia katika kukuza uchumi na kuwa endelevu na kuleta maendeleo ya kichumi na kuwa chachu ya maendeleo katika taifa.

Kaulimbiu ya kongamano hilo la sita la Jumuiya ya Afrika Mashariki la Usafiri wa Anga ni "Mustakabali wa Usafiri wa Anga: Kudumisha Mifumo ya Usafiri wa Anga yenye Ustahimilivu, Uendelevu, Ubunifu na Usalama".



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, (wa tatu kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa benki ya Exim, Stanley Kafu (kulia), alipotembelea maonyesho wakati wa maadhimisho ya Siku ya Msalaba Mwekundu Duniani, jijini Dodoma hivi karibuni. Kupitia mpango wake wa kijamii wa 'Exim Cares', imekuwa ikiunga mkono miradi mbalimbali katika sekta za afya, mazingira, elimu, ubunifu na masuala ya kifedha. Wengine ni Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar Katiba, Sheria, Utumushi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman (wa pili kulia) na Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 27 wanaswa tuhuma makosa ya kimtandao

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) limekamata watu 27 kwa tuhuma za kuhusika na makosa ya kimtandao, ikiwamo kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu katika Mkoa wa Dar es Salaam, Ifakara (Morogoro) na Sumbawanga (Rukwa).

Akizungumza jana Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema watuhumiwa hao wamekuwa wanapiga simu na kusambaza ujumbe fupi wa maandishi wakidai fedha imetumwa kimakosa, hivyo irudishwe.

Kamanda Muliro alieleza kuwa watuhumiwa wanadai wanasafisha nyota ili kupata utajiri na kuwaunganisha na kitu wanachodai 'freemason', kuwadanganya watu kuwa wameshinda na kupata gawio kutoka kampuni mbalimbali za simu na wengine hujifanya maofisa wa serikali na kuwa wanatatua shida za watumishi wenye matatizo, baadaye huishia kuwaibia watu fedha kwa njia ya mtandao.

"Katika ufuatiliaji wamekamatwa Pius Boniface (29), mkazi wa Eden A ambaye ni wakala wa kusajili laini za simu; Ezekiel Frank (30), mkazi wa Mikonko Mbalika ambaye ni dereva wa bodaboda na wengine 13, wote wakazi wa Sumbawanga.

"Pia amekamatwa Noel Panclas (37) 'Mkono wa Chuma', mkazi wa Muhola, Ifakara kwa tuhuma za kujifanya mtumishi kutoka Wizara ya Ulinzi na anaweza kuwapatia kazi vijana jeshini, hivyo wamtumie fedha akamilishe taratibu kuwasaidia," alisema Kamanda Muliro.

Wengine waliokamatwa ni Richard Masunga (23), mkazi wa Ifakara kwa tuhuma za kupiga simu akidai ni ofisa wa TCRA na kwamba laini ya simu ya mhusika imefungiwa kutokana na kutorasimisha usajili wake, hivyo humtajia mwathirika namba aingize kwenye simu yake ili laini ifunguliwe, baadaye huishia kuhamisha fedha za mhusika na kutenda kosa la wizi.

Mwingine ni Agrey Razaki (23), mkazi wa Mbassa, Ifakara anayeshikiliwa kwa tuhuma za kutuma ujumbe kwa watu kuwa wamejishindia vitu mbalimbali kama bajaji, bodaboda au gari, hivyo wampigie simu ili awapatie maelekezo ya jinsi ya kupata zawadi zao. Mhusika anapompigia huambiwa kuwa anatakiwa kulipia fomu ya kujiunga na mwishowe huibiwa.

Pia wamo Rahim Sangila (20), Festo Ndizi (27) na wenzao saba, wote wakazi wa Ifakara ambao wamekamatwa kwa tuhuma za kutuma ujumbe wa miamala ya fedha kwa watu mbalimbali na baadaye huwapigia simu kuwaeleza kuwa wao ni wafanyakazi wa kampuni husika ya simu na "kuna muamala umetumwa kimakosa", hivyo kuwataka kuurudisha.

"Watuhumiwa hao wamekamatwa wakiwa na jumla ya simu 41 na laini za simu 88 za mitandao mbalimbali na zenye usajili tofauti, wote watafikishwa mahakamani haraka iwezekanavyo kujibu tuhuma zinazowakabili," alisema Kamanda Muliro.

Alitoa hadhari kwa wananchi kuwa makini wanapopigiwa simu au kutumiwa ujumbe unaowaelekeza au kuwataka kutuma fedha kwa watu wasiowafahamu au kuwatilia shaka na kutolipia huduma wasizozifahamu kwa miamala ya simu.

"Wananchi wanahimizwa kutoa taarifa hizo polisi ili ufuatiliaji ufanyike haraka na watuhumiwa wakamatwe haraka, na wote watakaobainika watakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria," alisema.

# Serikali yataja kiini cha kuhamisha wananchi KIA

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI imetaja kiini cha kuwahamisha wananchi walioko katika kaya 1,712 za vijiji vinane vya mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, vilivyovamiwa na kuendeleza ardhi inayomilikiwa na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), kuwa ni vumbi kubwa la upepo wa kisulisuli linalotimka kuathiri miruko na utuaji wa ndege, kiasi cha ndege kushindwa kutua na kwenda nchi jirani.

Aidha, athari nyingine ni shughuli za kibinadamu kusababisha kuharibika kwa uoto wa asili kwa kukata miti, majani na kulisha mifugo, na pia kusababisha serikali kushindwa kutekeleza mpango wake mahususi kwa ajili ya kuendeleza uwanja huu.

Jana, wakati anatoa tamko la serikali kuhusiana na mgogoro wa ardhi, baina ya wananchi na uwanja huo wa KIA, Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alisema wananchi wa Wilaya za Hai na Arumeru, waliingia katika eneo hilo na kuweka makazi na kufanya shughuli za kibinadamu kati ya mwaka 2007 hadi 2010.

Kwa mujibu wa Matinyi, uwanja huo wa KIA ulianza kumilikiwa na serikali mwaka 1969, wakati huo ukiwa chini ya Pori Tengefu la Sanya Lelatema, lililokuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 800.

"Serikali ilitenga kilomita za mraba 110 kutoka kwenye hizo 800 mahususi kwa ajili ya ujenzi wa uwanja huu wa Kilimanjaro na baadae na eneo lilipimwa rasmi 1989 kwa ramani iliyokuwa na namba E 5255/18; na ikasajiliwa na kupewa namba 231264 na hatimaye hati ilipotoka ilianza kumilikiwa ikiwa na hati 22270.

"Eneo hili linapakana na vijiji vine ambavyo Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha ni Kaloleni, Samaria, Malula na Majengo Kati.

...Kwa upande wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro kuna vijiji vinne vinavyopakana na uwanja huu ambavyo ni Sanya Station, Tindigani, Chemka na Mtakuja."

Kwa mujibu wa Msemaji Mkuu wa Serikali, shughuli hizo za binadamu zilihusisha kilimo na ufugaji ndani ya uwanja, zinaathiri shughuli za uendeshaji hasa katika kipindi cha kiangazi; ambapo vumbi hutimka katika eneo ambalo ni kame kutokana na majani mengi kutumika kama malisho.

Vilevile, alisema hali hiyo imekuwa ikiathiri uono hafifu wa marubani, kiasi cha ndege wakati mwingine kushindwa kutua na kulazimika kwenda kwenye viwanja vya nchi jirani.

"Athari nyingine kutokana na shughuli hizo za kibinadamu ilikuwa ni pamoja na kuharibika kwa uoto wa asili kwa kukata miti, majani na kulisha mifugo, na pia kusababisha serikali kushindwa kutekeleza mpango wake mahusussi kwa ajili ya kuendeleza uwanja huu.

Katika taarifa hiyo ya serikali, Wilaya ya Arumeru, wananchi wamelipwa fidia zaidi ya Sh. bilioni 4.042, wakati Wilaya ya Hai wananchi wamelipwa Sh. bilioni 7.27 zilizojumuisha fidia ya majengo, mazao ya kudumu, posho ya makazi, posho ya usafiri, posho ya usumbufu na posho za makaburi.

Kadhalika, alisema hadi kufikia Mei 14, mwaka huu, wananchi 46 pekee ndio hawajalipwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kukosa akaunti za benki, majina kutofautiana katika taarifa za malipo na yaliyopo benki.

Pia, tatizo jingine ni kukosekana kwa uthibitisho wa mirathi kwa wananchi wanaotakiwa kulipwa fidia na baadhi ya wananchi kufungua mashauri ya madai Mahakama Kuu, kupinga zoezi la ulipaji linaloendelea.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Amiri Mkalipa, alisema kazi ya kuwaondoa wananchi hao imeathiri pia maeneo kadhaa ya serikali, ambayo ni Shule ya Msingi Tindigani, itakayohamishwa kutoka Kitongoji cha Tindigani kwenda Kitongoji cha Bonza.

Wakati, Zahanati ya Tindigani, itaihamishwa kutoka Tindigani kwenda Bonza.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Tindigani, Richard Moringe, alipozungumza na Msemaji Mkuu wa Serikali, aliomba serikali isogeze huduma za afya na elimu, kwakuwa wananchi watalazimika kuzifuata umbali wa kilomita tano walipohamia.

ASASI ZA KIRAIA

Asasi za kiraia na zenye kutetea haki za binadamu na ardhi, Mei 9, mwaka huu, zilitoa tamko zikitaka serikali isitishe mara moja operesheni ya kuwahamisha kwa nguvu wakazi wa vijiji jirani na uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro.

Katika taarifa yao, serikali kupitia barua mbalimbali kabla ya mwaka 2006 ilikiri kufahamu mgogoro huo.

Mbunge wa Hai wakati huo, Freeman Mbowe aliufikisha Bungeni mgogoro huo Aprili 20, 2003.

Kutokana na mgogoro huo, asasi hizo zimemtaka Rais Samia Suluhu Hassan, kufanya yafuatayo;

Asitishe mara moja uhamishaji huo, apeleke msaada wa kibinadamu kwa waathirika walioachwa bila makazi na chakula na aunde tume huru kuchunguza jambo hilo.

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**ALICE PATRICK LIHUNDI** anatangaza kupotea kwa Pikipiki zenye namba za usajili **MC 141 CDH na MC 446 CMF.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote che polisi.

Control No. **9910841100922.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 7975/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late JULIUS ALOYCE LYMO of Mpwayungu Chamwino Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ESTER LAZARO MGUNDULWA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 16 Day of 5, 2024

Date at Dodoma this 16 Day of APRIL, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**STEPHEN WILBARD MSECHU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T139CLQ** aina ya Suzuki ESCUDO , Chassis No. **TD01W118331,** Engine No. G16A258935. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/13791/2024**

## HABARI KIMATAIFA

# Misri, Israel zavutana kufungwa kwa mpaka

**CAIRO,** Misri

NCHI za Israel na Misri ziko kwenye mvutano kuhusu mpaka wa Rafah, zikilaumiana baada ya kuendelea kufungwa wakati ikishuhudiwa hali mbaya ikizidi kuhatarisha maisha ya binadamu Ukanda wa Gaza.

Vikosi vya Israel vimeudhibiti upande wa pili wa mpaka huo siku ya Jumanne.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Israel, Israel Katz, aliziambia nchi za Uingereza na Ujerumani kwamba kuna haja ya kushawishi Misri kufungua tena mpaka huo.

Hata hivyo, Misri ilisema kuwa operesheni za kijeshi za Israel katika eneo hilo zinazuia misaada kuingia ndani ya gaza.

Uongozi wa Misiri ulieleza kwamba Israel inajaribu kuelekeza lawama upande wao kuhusu kuzuiliwa kwa misaada hiyo, jambo ambalo sio kweli.

Waziri Katz alisema kundi la wapiganaji la Palestina Hamas, haliwezi tena kudhibiti mpaka wa Rafah, kwa sababu hawawezi kuvumilia hofu ya kiusalama.

"Ulimwengu unaweka jukumu la hali ya kibinadamu kwa Israel, lakini umuhimu wa kuzuia janga la kibinadamu huko Gaza sasa liko mikononi mwa marafiki zetu wa Misri, alisema Katz kupitia mtandao wa X.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Misri, Sameh Shoukry, alijibu haraka lawama hizo kwa kueleza kwamba Israel inahusika na mgogoro wa kibinadamu ndani ya Gaza kutokana na hatua za jeshi la Israel katika eneo la Rafah.

Misri imekuwa moja ya wapatanishi katika mazungumzo yaliyokwama ya kusitisha mapigano, lakini uhusiano wake na Israel umekuwa mbaya tangu Israel ilipoteka upande wa pili wa mpaka wa Rafah, Mei 7, mwaka huu.

Tangu eneo la Rafah kuvamiwa na vikosi vya Israel, Wapalestina 450,000 wamekimbia wiki iliyopita na kwenda maeneo mengine ya Ukanda wa Gaza.

Vifaru vya Israel vinaripotiwa kuingia ndani zaidi katika mji huo ulioko kaskazini mwa mpaka huo.

Wakati huo huo, serikali ya Marekani imeliambia bunge la Congress kuwa inataka kupeleka silaha nchini Israel zenye gharama ya dola bilioni moja.

Kulingana na shirika la habari la Reuters, kifurushi hicho kitajumuisha silaha, chokaa na magari ya kivita.

Mpango huo, uliothibitishwa na kupatiwa CBS, lazima uidhinishwe na wabunge.

Wiki iliyopita Rais Joe Biden, alisema kuwa atasitisha usafirishaji wa silaha kwenda Israel ikiwa itaanzisha uvamizi kamili katika mji wa Rafah.

Rais Biden alisema alichelewesha usafirishaji wa mabomu yenye thamani ya dola 2,000 kwenda Israel kwa sababu yanaweza kutumika katika operesheni hiyo ya ardhini.

Alipoulizwa na CNN kuhusu ucheleweshaji huo, kiongozi huyo alisema kuwa raia wameuawa Gaza kutokana na mabomu hayo.

Msaada huo ni wa kwanza tangu utawala wa Biden kusitisha uhamishaji wa silaha kwenda Israel wiki iliyopita.

Siku ya Ijumaa, ripoti ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani iligundua kuwa baadhi ya silaha za Marekani zilizotolewa kwa Israel huenda zilitumika kinyume na sheria za kimataifa.

Ingawa ripoti hiyo ilikuwa ni karipio la wazi la baadhi ya operesheni za Israel katika Ukanda wa Gaza, ilimaliza kwa kusema kwamba kampeni ya Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) ilikiuka sheria za kimataifa.

**BBC**

# Kiongozi upinzani azuiwa kugombea urais Rwanda

**KIGALI,** Rwanda

MAHAKAMA ya nchini Rwanda imekataa rufani ya mwanasiasa wa upinzani, Bernard Ntaganda (55) ambaye alipinga hukumu ya awali ya kuzuiwa kugombea nafasi ya urais.

Ntaganda, ambaye anatoa upinzani mkali kwa Rais Paul Kagame, aliiomba Mahakama Kuu kubatilisha hukumu iliyotolewa muongo mmoja uliopita ambayo imemzuia kushiriki uchaguzi mkuu utakaofanywa Julai mwaka huu. Majaji watatu kwa pamoja walikataa rufani ya Ntaganda, wakisema kwamba mwanasiasa huyo hakulipa kiasi cha faranga 106,000 za Rwanda kama ada ya kesi ya awali.

"Mahakama Kuu imehitimisha kuwa Bernard Ntaganda alishindwa kufuata sheria inayowataka watu binafsi kutaka kubatilishwa kwa hukumu zao, na hivyo mahakama inakataa rufani yake," ilisema hukumu hiyo.

Ntaganda, ambaye ni wakili na mwanzilishi wa chama cha PS-Imberakuri, alieleza kuwa ana uthibitisho wa malipo ya ada hizo na hashangazwi na uamuzi huo wa mahakama.

Kiongozi huyo ni wa pili wa upinzani kuzuiwa kushiriki katika uchaguzi huo dhidi ya Paul Kagame. Mwezi Machi, mpinzani mwingine wa muda mrefu, Victoire Ingabire, alifungwa jela mwaka 2013 na kumzuia kugombea. **RFI**



Wakazi wa mji wa Kharkiv nchini Ukraine wakitembea juu ya kifusi baada ya jengo la ghorofa kuharibiwa na shambulio la kombora kutoka vikosi vya Russia juzi. **PICHA: AFP**

# Ali Bongo na wanawe wagoma kula

**LIBREVILLE,** Gabon

RAIS wa zamani wa Gabon, Ali Bongo, ambaye aliyeondolewa madarakani na jeshi na wanawe wawili wamegoma kula na wakilalamika kufanyiwa vitendo vya kikatili.

Mawakili wa familia hiyo walisema kuwa kiongozi huyo na watoto wake Jalil na Bilal wameitisha mgomo huo kutokana na serikali ya kijeshi kuwapa mateso wakiwa kwenye kizuizi cha nyumbani.

Bongo aliondolewa madarakani katika mapinduzi ya kijeshi yaliyofanyika mwezi Agosti mwaka jana, muda mfupi baada ya kushinda kura ya urais iliyoibua mgogoro wa kisiasa.



Baada ya mapinduzi hayo, Bongo na familia yake walizuiwa kwenye makazi yake yaliyoko katika mji mkuu, Libreville.

Serikali hiyo pia iliwashikilia mkewe Sylvia Bongo na mwanawe mkubwa Noureddin, wakisubiri kufikishwa mahakamani kwa tuhuma za rushwa.

Katika taarifa ya mawakili wao walidai kuwa Noureddin na Sylvia walipigwa na kunyongwa wakiwa kizuizini.

Pia wanadai kuwa Noureddin aliteswa, kuchapwa viboko na hata kupigwa na shoti ya umeme.

Rais huyo aliyeondolewa madarakani, mwenye umri wa miaka 64, aliongoza nchi hiyo yenye utajiri mkubwa wa mafuta tangu 2009 aliporithi kutoka kwa baba yake ambaye amekuwa madarakani kwa zaidi ya miaka 40.

Mawakili wa familia hiyo walisema wamewasilisha malalamiko katika mahakama ya Paris, wiki moja kabla ya kiongozi wa serikali ya Gabon, Brice Oligui Nguema kufanya ziara nchini humo.

**BBC**

# SERIKALI YAIBEBA CHANETA IKITAKA 'MAKUBWA' AFRIKA

**Na Shufaa Lyimo**

SERIKALI imetoa Sh. milioni 10 kwa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA) kwa ajili ya kuendesha mashindano ya Klabu Bingwa Afrika yanayoendelea kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mashindano hayo juzi jioni, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, alisema serikali imetoa fedha hizo ili kuhakikisha timu ya Tanzania inafanya vizuri katika mashindano hayo.

Msigwa alisema anaamini fedha hizo zitaongeza morali kwa wachezaji na hatimaye kupambana ili kulibakisha kombe la michuano hiyo nyumbani.

"Fedha tutakazowakabidhi tunataka kuona zinazaa matunda katika mashindano hayo, sitawaelewa nikiona hamfanyi vizuri, ugomvi wenu na mimi bado haujaisha kwa sababu bado hamjafika ninapotaka mfike," alisema Msigwa.

Katibu huyo alisema awali mchezo huo uliyumba kutokana na migogoro iliyokuwapo ndani ya chama hicho na kuongeza kwa sasa anafarijika kuona uongozi unapambana kuhakikisha mchezo huo unafika mbali zaidi.

"Mwakani nataka nione timu zinaongezeka zaidi pamoja na kuandaa mashindano ya ndani yatakayotufanya tonekane tumekuwa kupitia mchezo huu kama ilivyo katika nchi ya Uganda," alisema katibu huyo.

Naye Mwenyekiti wa CHANETA, Dk. Devotha Marwa, alisema amefurahi serikali kuwaunga mkono na kuahidi watahakikisha wanautendea haki mchezo huo.

Marwa aliahidi wataendelea kupambana kuhakikisha mchezo huo unapata maendeleo kama kauli ya kiongozi huyo wa serikali ilivyoelekeza.

"Nimefarijika baada ya Katibu kuonyesha moyo wa kutusaidia fedha hizo, ninaahidi kufanya kila linalowezekana ili kuukuza mchezo huu ambao utasaidia wachezaji kupata ajira nje ya nchi, vile vile hujenga afya," alisema Marwa.

Mashindano ya Klabu Bingwa Taifa yanatarajiwa kumalizika Mei 18, mwaka huu na yameshirikisha timu 12 kutoka nchi za Uganda, Kenya na Zanzibar.




Mshindi wa Kampeni ya Bima Kitonga, Amani Mbise (katikati), akishuhudia gari lake likijazwa mafuta katika Kituo cha Puma jijini Dar es Salaam baada ya kuibuka kidedea katika shindano lililoendeshwa na Kampuni ya Sanlam General iliyoshirikiana na Selcom Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kagame Cup kufanyika nchini

**Na Somoe Ng'itu**

MASHINDANO ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame yamepangwa kufanyika kuanzia Julai 20 hadi Agosti 4, mwaka huu imefahamika.

Mara ya mwisho mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yalifanyika mwaka 2021 na Express ya Uganda ilitwaa ubingwa huo baada ya kuifunga Big Bullets kutoka Malawi bao 1-0 katika mechi ya fainali.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa CECAFA, Auka Gecheo, alisema nchi zote 12 wanachama wa baraza hilo wanatarajiwa kushiriki mashindano hayo pamoja na timu nyingine nne zitakazoalikwa.

„Tunafuraha kutangaza kurejea tena kwa mashindano haya, tunaamini itasaidia kuzipa timu zetu maandalizi mazuri kuelekea msimu mpya 2024/2025 wa michuano ya kimataifa ya CAF," alisema Auka.

Aliongeza maandalizi ya mashindano ya Kombe la Chalenji yatakayofanyika Zanzibar yanaendelea vizuri na CECAFA imeamua kurejesha michuano hiyo pia ili kutoa nafasi kwa timu kujiandaa na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika Septemba, mwaka huu.

Kagame Cup ilipoteza ushindani wake baada ya timu vigogo kujitoa kushiriki kwa madai ya kubanwa na maandalizi ya msimu mpya.

Rais wa Rwanda, Paul Kagame, amekuwa mdhamini mkuu wa mashindano hayo maarufu katika ukanda huu kwa kutoa zawadi kwa washindi.

## Geita Gold FC na dakika 450 ngumu

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Geita Gold imecheza mechi tano za Ligi Kuu Tanzania Bara, sawa na dakika 450 bila kupata bao, huku pia ikicheza mechi saba, sawa na dakika 630 bila kupata ushindi wowote.

Takwimu hizo zimekuja, baada ya juzi kulazimishwa suluhu nyumbani kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Geita dhidi ya Coastal Union.

Geita Gold ambayo sasa iko nafasi ya 15 katika msimamo wa ligi, haijafunga bao lolote tangu Aprili 13, mwaka huu, ilipotoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Mtibwa Sugar, baada ya hapo imetoka suhuhu tatu dhidi ya Prisons, Tabora United na ya juzi dhidi ya Coastal Union, ikachapwa mabao 2-0 dhidi ya JKT Tanzania na Namungo.

Mbali na hilo, timu hiyo imecheza mechi saba bila kupata ushindi, mara ya mwisho kufanya hivyo ilikuwa, Machi 7, mwaka huu ilipoifunga Dodoma Jiji bao 1-0, baada ya hapo ikachapwa goli 1-0 na Yanga, na ikafuatia sare ya mabao 2-2 dhidi ya Mtibwa Sugar.

„Tunatengeneza nafasi lakini hatuzitumii, tuna tatizo la kuweka mpira wavuni, hata mechi zilizopita, tumekuwa tukiwamiliki wapinzani wetu, lakini tatizo letu ni kufunga," Denis Kitambi, Kocha Mkuu wa timu hiyo alisema.

## JKU SC, Zimamoto zatinga nusu fainali

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU na Zimamoto zimeungana na Uhamiaji FC pamoja na Mlandege kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la ZFF (FA CUP).

JKU imefanikiwa kutinga hatua hiyo baada ya kuwaondoa Taifa Jang'ombe FC kwa penalti 4-2 baada ya dakika 90 kumalizika kwa kutoshana nguvu ya sare ya bao 1-1.

Zimamoto yenyewe imesonga mbele baada ya kuwafunga Mafunzo bao 1-0 michezo yote imechezwa jana kwenye viwanja vya Mau A na B.

Kocha Mkuu wa JKU, Salum Haji, alisema haikuwa kazi rahisi kufikia hatua ya nusu fainali kutokana na michuano hiyo kuwa migumu hasa wanapocheza dhidi ya timu za madaraja ya chini.

"Mashindano haya ni magumu sana, hakuna asiyeyajua, kwa sababu kila mtu inataka kuhakikisha inasonga mbele zaidi michuano hii na hakuna mechi ya marudiano, inamaana ukifungwa ndio umepoteza," alisema kocha huyo.

Bingwa wa michuano hii ataiwakilisha Zannzibar katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BRUNO ATAKIWA BAYERN
BAYERN Munich imeonyesha nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Manchester United, Bruno Fernandes, msimu huu wa joto na inaamini inaweza kumpata mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 29. (***Independent***)

### NYOTA WAMTAKA TUCHEL
WACHEZAJI wa Bayern Munich akiwamo mshambuliaji wa England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 30, wanataka Kocha, Thomas Tuchel, kubadili uamuzi wake wa kuondoka katika klabu hiyo ya Bundesliga mwishoni mwa msimu huu. (***Abendzeitung***)

### BRANTHWAITE ANUKIA UNITED
KLABU ya Manchester United iko tayari kutoa pauni milioni 55 ili kumnunua beki wa Everton na Timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite. (***Daily Mail***).

### FRIMPONG NJIA MOJA
MLINZI wa Uholanzi, Jeremie Frimpong, mwenye umri wa miaka 23, anaelekea kuondoka Beyer Leverkusen msimu huu wa joto huku Real Madrid, Manchester City, Arsenal na Manchester United zikiwa na nia ya kunufaika na kipengele cha pauni milioni 35 katika mkataba wake. (***Bild***)

### ARSENAL, CITY VITANI TENA
ARSENAL na Manchester City zimewasiliana na kiungo wa kati wa Newcastle United na Brazil, Bruno Guimaraes, mwenye umri wa miaka 26, kuhusu uwezekano wa uhamisho msimu wa joto. (***Caughtoffside***)

### FRANK KUMRITHI TEN HAG
KOCHA wa Brentford, Thomas Frank ni miongoni mwa makocha wanaotarajiwa kujiunga na Manchester United endapo mabosi wa timu hiyo wataamua kumfuta kazi, Erik ten Hag. (***Telegraph***)

### NAPOLI YAMTAKA CONTE
NAPOLI itampa kocha wa zamani wa Chelsea na Tottenham Hotspur, Antonio Conte, pauni milioni 5.6 kwa mwaka endapo mwalimu huyo atakubali kutua hapo ingawa nia ya AC Milan ya kumnunua Mtaliano huyo mwenye umri wa miaka 54 imefifia. (***Sport Italia***)

### ROYAL KUTUA AC MILAN
AC Milan inamsaka beki wa Tottenham Hotspur mwenye umri wa miaka 25, ambaye ni raia wa Brazil, Emerson Royal. (***Fabrizio Romano***)

### ADARABIOYO SOKONI EPL
MANCHESTER United ipo katika mbio moja na Newcastle United kuwania kumsajili beki wa Fulham, Tosin Adarabioyo, mwenye umri wa miaka 26. (***Talksport***)

### THURAM ATAJWA LIVERPOOL
LIVERPOOL imepewa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Nice na Ufaransa, Khephren Thuram, mwenye umri wa miaka 23 kwa dau la pauni milioni 13 msimu huu. (***Mirror***)

### SLOT KUMVUTA HULSHOFF
KOCHA wa Feyenoord, Arne Slot, anapanga kumfanya kocha wake msaidizi, Sipke Hulshoff, kwenda nae Liverpool atakaporithi mikoba ya Jurgen Klopp. (***ESPN***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AWATAKA NYOTA WAKE KUTULIA

**LONDON,** England

●●● Kocha huyo asema ubingwa ni wa City na watautangaza Jumapili...

PEP Guardiola amewaambia wachezaji wake wa Manchester City "tulieni" katika mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu England dhidi ya West Ham utakaochezwa Jumapili na watanyanyua taji lao la nne mfululizo.

**Mabao mawili ya kipindi cha pili kutoka kwa Erling Haaland yaliihakikishia Manchester City ushindi wa 2-0 dhidi ya Tottenham Hotspur hapu juzi usiku na kusogea mbele ya Arsenal na kuweka mbio mikononi mwao siku ya mwisho.**

"Walikuwa wakichezea matokeo katika kipindi cha kwanza," alisema Guardiola.

"Unapofanya hivyo utapoteza Ligi Kuu. Huwezi kufanya kwa kiwango chako.

"Hao ni binadamu, ninaelewa presha, hata Arsenal walicheza vizuri dhidi ya Manchester United, walijua wasiposhinda pale hawatashinda Ligi Kuu.

"Itakuwa sawa Jumapili kwetu dhidi ya West Ham. Tutahisi shinikizo.

"Ndio maana tunazungumza na kusema kila mtu anapaswa kupumzika na kufanya kile anachopaswa kufanya, ni hivyo tu".

City watashinda ligi kwa kuifunga West Ham bila kujali Arsenal watapata matokeo gani dhidi ya Everton na Guardiola aliongeza: "Tunajua tunachochezea.

Mvutano upo, mpinzani ni mzuri sana. Ndio maana ni ngumu, tunajua hilo.

"Kila mtu aje uwanjani na kupiga kelele. Michezo hii ni migumu zaidi lakini inabidi ufanye hivyo. Tutakuwa na siku moja ya mapumziko, siku mbili za kujiandaa, halafu tutafanya kila tuwezalo".

# TEN HAG KUTOAGA UNITED



**MANCHESTER,** England

ERIK Ten Hag amesema hatawaaga mashabiki wa Manchester United baada ya mechi yao ya mwisho ya nyumbani msimu huu licha ya kutokuwa na uhakika kuhusu nafasi yake kama kocha.

Lakini Mholanzi huyo alisisitiza haitakuwa kwaheri kwake, licha ya kutokuwapo kwa uwazi iwapo atasalia klabuni hapo baada ya majira ya kiangazi.

„Kwaheri? Kwangu? Sio jinsi ninavyohisi na jinsi ninavyoiona," alisema Ten Hag akiwaambia wanahabari juzi.

„Sio jinsi ninavyoenda kuanza mzunguko huo wa heshima kwa mashabiki, hapana. Kupitia nyakati nzuri na mbaya tuko pamoja na mashabiki wanaonesha hilo, tuko pamoja."

Mmiliki mwenza mpya wa United, Sir Jim Ratcliffe bado hajatoa taarifa kwa umma kuhusu hatima ya Ten Hag huku uamuzi ukiwekwa baada ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City itakayochezwa Mei 25, mwaka huu.

Ten Hag amesimamia msimu mbaya, ambao unakaribia kuwa mwisho mbaya zaidi wa Ligi Kuu kwa United, lakini kocha huyo mwenye umri wa miaka 54 alisema bado anaungwa mkono na mashabiki wengi.

„Kweli ndio," alisema.

„Uwanjani, ugenini na nyumbani, huwa wanaiunga mkono timu na kuniunga mkono. Pia nikiwa mitaani, wengi wanakuja kwangu.

„Sijapata maoni hasi kwa sababu mashabiki wanaelewa tulipo. Mashabiki wanaelewa klabu hii iko katika kipindi cha mpito na mashabiki wanaelewa matatizo makubwa ambayo tumekabiliana nayo na hasa nafasi katika maeneo muhimu."

# Bayern Munich watupa ndoano kwa Fernandes



**MANCHESTER,** England

BAYERN Munich wametajwa kuanzisha mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Manchester United, Bruno Fernandes, huku ripoti ikidai wachezaji wenzake wa kimataifa wa Ureno wanahofia huenda akahama msimu huu wa joto.

Mustakabali wa Fernandes umekuwa na uvumi mkubwa tangu iliporipotiwa United iko tayari kusikiliza ofa kwa kila kiungo kando na Rasmus Hojlund, Kobbie Mainoo na Alejandro Garnacho.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 alichochea ‚moto' huo kwa kukiri hadharani anaweza kufikiria hatima yake katika klabu hiyo msimu huu wa joto, ingawa Kocha, Erik ten Hag, alisisitiza haraka maoni ya Fernandes yameondolewa katika muktadha na mauzo ya msimu wa joto hayakuwa mezani.

Sasa, hali ya sintofahamu kuhusu mustakabali wa Fernandes imeibuka tena huku gazeti la The Independent likidai anawaniwa na Bayern Munich msimu huu wa joto.

Bayern Munich inasemekana inaamini Fernandes anaweza kufikiwa msimu huu wa joto kwa kuwa hafanani na wasifu wa kikosi cha United kinachojengwa upya.

Habari za Manchester Evening zinaongeza baadhi ya watu ndani ya chumba cha kubadilishia nguo cha Old Trafford wanashaka Fernandes bado atakuwa kwenye klabu hiyo msimu ujao, huku ripoti ikidai huenda akaondoka katika kipindi hiki.

Inasisitizwa Fernandes hataki kabisa kuondoka United na angefurahi zaidi kusalia.

Ten Hag alifanya kila awezalo kujaribu kukomesha uvumi huo alipoulizwa kuhusu mustakabali wa Fernandes wakati wa mkutano na waandishi wa habari Jumanne.

„Ni swali sawa na wiki iliyopita. Kwa hivyo nilijibu," alisema Yen Hag.

„Sasa na kwa miaka yote aliyokuwa United alikuwa mchezaji muhimu sana kwa Man United na kutengeneza nafasi nyingi zaidi katika Ligi Kuu, asisti nyingi, mabao mengi. Ni wazi ni mchezaji muhimu sana kwetu."

# Enzo: Nimeiumiza Chelsea

**LONDON,** England

KIUNGO wa kati wa Chelsea, Enzo Fernandez, amekiri „nilikuwa nikiiumiza timu" alipokuwa akijaribu kucheza huku akiwa na maumivu ya henia.

Fernandez alichukua uamuzi wa kufanyiwa upasuaji mwezi uliopita baada ya wiki kadhaa za kukosolewa vikali kuhusu uchezaji wake akiwa na Chelsea, ambao hawajafungwa tangu nyota huyo wa kimataifa wa Argentina alipopigwa kisu.

Akizungumza na DSports, Fernandez alifichua ni muda gani jeraha hili limekuwa likiathiri kiwango chake uwanjani.

„Nilikuwa nikicheza na maumivu na sindano kwa miezi nane," alisema Fernandez.

„Nililazimika kufanya uamuzi wa kufanyiwa upasuaji, lilikuwa jambo bora zaidi. Nilikuwa nikiidhuru timu na sikutaka kujiweka wazi.

„Sijambo, watu wanaweza kustarehe. Nazidi kuwa bora siku hadi siku, na nina hamu ya Copa America kufika. Tayari nimeanza mazoezi ya uwanjani, ahueni ni ya juu, na nina matumaini kufanya mazoezi na timu ya taifa hivi karibuni ninafuraha sana kwa Copa America hii, itakuwa mara yangu ya kwanza kucheza ndani yake.



Fernandez pia alitumia fursa hiyo kuonyesha uungwaji mkono wake kwa Kocha, Mauricio Pochettino, ambaye matumizi ya kiungo huyo pia yamezua maswali msimu huu.

„Nilipofika, kulikuwa na fujo, kulikuwa na wachezaji wengi," alisema.

„Mauricio alitoa utaratibu na utambulisho kwa timu. Maadili ya kazi ni tofauti.

„Alibadilisha kila kitu, na ukweli ni mzuri. Timu iko makini zaidi na inafanya kazi kwa bidii. Hiyo ni muhimu kwa siku hadi siku, na wikendi ikija, unaweza kuona tofauti."

Fernandez hatarejea Chelsea msimu huu lakini ana matumaini ya kucheza katika michuano ya Copa America msimu huu wa joto na hata anataka apewe ruhusa ya kuiwakilisha Argentina katika Michezo ya Olimpiki.

„Nina uwezekano wa kwenda na ningependa kwenda katika Michezo ya Olimpiki," Fernandez alikiri. „Ni uamuzi wa Chelsea na bado sijazungumza nao kuhusu hilo."

HABARI MICHEZO

# SERIKALI KUTOA TUZO ZA WANAMICHEZO JUNI 9

Na Saad Akida

WIZARA ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) imeandaa Tuzo za Wanamichezo Bora zitakazofanyika Juni 9, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Super Dome uliopo Masaki, Dar es Salaam.

Tuzo hizo ni mara ya pili kufanyika kwa mwaka huu baada ya mwaka jana kufanyika Machi 17, 2023, kwenye ukumbi, Mlimani City kwa kupata Mwanamichezo bora wa 2022.

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Mwenyekiti wa BMT, Leodegar Tenga, alisema dhamira ya kutoa tuzo hizo ni kuwaenzi na kuwaheshimisha wanamichezo kwa kufanya vizuri ndani ya michezo ya kanda, Afrika na mashindano ya dunia.

Tenga alisema faida kubwa katika tuzo hizo ni kuchagiza maendeleo ya michezo ikiwamo kuongeza viwango vya wachezaji katika kupambana kufikia mafanikio.

"Tunatoa tuzo kwa wanamichezo wanaofanya vizuri ndani na nje ya mipaka ya Tanzania kwa kuipeperusha vyema bendera ya Taifa. Sasa hivi nchi yetu sio kichwa cha mwendawazimu kwa sababu timu zote zimejipanga.

Ni miaka mingi sana kuona timu mbili kuingia robo fainali kama ilivyo kwa Simba na Yanga, hii kazi nzuri kwa uongozi, makocha na wachezaji," alisema Tenga.

Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo, Mkumbukwa Mtambo, alisema hii ni mara ya pili kuandaa tuzo hizo na mwaka huu watatoa tuzo za jumla na si kwa kila mchezo.

„Mabadiliko haya yanalenga kuongeza ushindani na ufanisi ikiwa ni pamoja na kuleta usawa wa uthamani kwa michezo yote, kadhalika mabadiliko haya yataongezea thamani tuzo hizi," alisema Mtambo.

Alitaja vipengele vilivyoongezeka ni cha Kocha Bora, Mwamuzi Bora na lengo la maboresho ni kuendelea kuhakikisha wadau wote muhimu katika tasnia ya michezo wanatambuliwa.

Aliongeza katika kuhakikisha mchakato wa utoaji tuzo unafanyika kwa uwazi, weledi na umakini, vyama na mashirikisho yote ya michezo nchini yameshirikishwa katika uteuzi wa wanamichezo bora.

Alitaja tuzo nyingine zitakazotolewa ni ya Mwanamichezo Bora Kijana wa Kiume na Kike, Mwanamichezo Bora wa Kiume na Kike mwenye Ulemavu, Timu Bora (Timu za Taifa), Kocha Bora wa Kiume na Kike, Mwanamichezo Bora wa Kiume na Kike kutoka mashindano ya shule, Mwamuzi Bora wa Kiume na Kike, Mwanahabari za Michezo Bora wa Kiume na Kike.



Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leodegar Tenga, akitambulisha kuwapo kwa Tuzo za Wanamichezo Bora zitakazofanyika Juni 9, mwaka huu jijini, Dar es Salaam. Kulia ni Katibu wa kamati ya tuzo hizo ambaye pia ni Katibu Mtendaji wa BMT, Neema Msitha na Mjumbe, Christina Koroso. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

## Diarra, Matampi wafungana

Na Adam Fungamwango

KIPA raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo wa Coastal Union, Ley Matampi, amefikisha idadi ya mechi 13 alizokaa langoni bila kuruhusu bao katika mechi za Ligi Kuu inayoelekea ukingoni, akimfikia Djigui Diarra wa Yanga.

Matampi, ambaye tetesi zinasema anawaniwa na Simba, amefikisha ‚clean sheets' 13, baada ya kutoruhusu wavu wake kuguswa katika mechi ya juzi walipocheza dhidi ya Geita Gold FC kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Geita.

Awali, Diarra, raia wa Mali, alikuwa anaongoza, huku mwenzake akiwa na ‚clean sheets' 12, lakini alishindwa kuongeza baada ya kuruhusu bao katika mechi ya Jumatatu iliyopita, ikichezwa, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro, timu yake iliposhinda mabao 3-1.

Matampi, aliyesajiliwa msimu huu akitokea klabu ya Renaissance ya DR Congo, amekuwa katika kiwango cha hali ya juu akicheza kwa mara ya kwanza, Ligi Kuu Tanzania Bara kiasi cha kuivutia Simba.

„Tunamhitaji kipa huyu, ni mzuri sana, kama anacheza katika klabu ya kawaida kama Coastal Union, tukimpata sisi, na tutakuwa tumefanya usajili wa mabeki bora, atakuwa kwenye kiwango cha juu zaidi kuliko hata hapa alivyo," kilisema chanzo chetu.

Baada ya Yanga kutwaa ubingwa, hivi sasa vita iliyobakia ni ya kumaliza msimu katika nafasi ya pili huku hekaheka nyingine ikiwa ni kupambana kusalia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Stephane Aziz Ki wa Yanga na Feisal Salum na Azam, kila mmoja akiwa na mabao 15, wao wako katika vita ya kuwania kiatu cha dhahabu huku mchezaji anayeongoza kwa kutoa pasi nyingi za mabao akiwa ni Aziz Ki akifuatiwa na Kipre Junior wa Azam FC.



## Nyota wa Mazembe atua Yanga

INATOKA UKURASA 24

mo wa kisasa wa uendeshaji.

"Pia tutakuwa na makubaliano rasmi ya urafiki wa kushirikiana kati ya klabu yetu ya Yanga na TP Mazembe ili kubadilisha ujuzi wa mambo mbalimbali ya kimpira yatakayosaidia timu," alisema Simon.

Yanga pia inaendelea kukamilisha mchakato wa kusajili wachezaji wake ambao mikataba yao imemalizika au inaelekea ukingoni.

## Simba yakomaa na Tchakei

INATOKA UK. 24

baada ya uhamisho wake wa kujiunga na Wekundu wa Msimbazi kushindikana, hivyo waajiri wake wakaamua ‚kumbana' ili asiondoke bure baada ya msimu huu kumalizika.

"Tunajua Simba wanamhitaji, na wamezungumza naye na yeye anahitaji kwenda huko, tulichofanya ni kumwongeza mkataba ili asiondoke bure, angalau na sisi tuambulie chochote," kilisema chanzo kutoka Ihefu.

Mchezaji huyo alijiunga na Singida Fountain Gate mwanzoni mwa msimu akitokea AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), kabla kuhamishwa na kupelekwa Ihefu, amekuwa katika kiwango cha hali ya juu na mwenye mchango kwa timu yake.

Nyota huyo amefunga mabao tisa msimu huu akiwa na timu zote mbili.

Wakati huo tetesi zinasema Simba ipo katika hatua za mwisho za kumalizana na mchambuzi wa video na viwango, Alexander Kerveillant kutoka Al Nassry ya Saudi Arabia kwa ajili ya kufanya kazi hiyo kuelekea msimu ujao wa mashindano.Mchambuzi huyo raia wa Ufaransa anatajwa kurithi mikoba ya Culvin Mavunga ambaye amekuwa na kikosi hicho kwa muda mrefu sasa.



Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema hiki ni kipindi cha tetesi za usajili, na haizuiliki, lakini ukweli na kila kitu kitafahamika pale Ligi Kuu Tanzania Bara itakapomalizika.

"Siku zote huwezi kuzuia tetesi za usajili, ila sisi ni kweli tutasajili, tena usajili mkubwa tu, nani tutamsajili, ni kiasi cha kusubiri, Simba tumekuwa na utaratibu wetu wa kumtangaza kila anayekuja katika klabu yetu," alisema Ahmed.

# Michezo

Alhamisi Mei 16, 2024

Nipashe




Ten Hag kutoaga United UK. 22



Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Tottenham Hotspur katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur ulioko London juzi usiku. City ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yakomaa kumnasa Tchakei

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumkosa katika dirisha dogo la usajili lililofungwa Januari, mwaka huu, Klabu ya Simba imeacha tena mchakati wa kusaka huduma ya winga na kiungo mshambuliaji wa Ihefu, raia wa Togo, Marouf Tchakei.

Simba imepania kwa kiasi kikubwa kufumua kikosi chake na kutengeneza timu mpya yenye ushindani kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano, inapiga hodi kwa kiungo huyo ambaye anacheza namba moja na Clatous Chama.

Habari kutoka ndani ya Simba zinasema huenda safari hii wanaweza nyota huyo kirahisi kutokana na kilichoelezwa pia nyota huyo yuko tayari kupata changamoto mpya lakini bado anabanwa na mkataba wake.

Chanzo chetu kingine kutoka Ihefu kimesema bado ana mkataba, hivyo kama Simba inamhitaji italazimika kufanya mazungumzo.

"Tulimhitaji dirisha dogo la usajili, lakini ilishindikana, klabu yake iliweka ngumu lakini mwenyewe alikuwa radhi kujiunga na timu yetu, akatuambia tusubiri msimu uishe atakuwa huru, sisi tunasimamia pale pale, lakini kama itakuwa vinginevyo basi tutaangalia itakavyokuwa lakini ni lazima tumng'oe, tumejidhihirisha ni mchezaji mzuri na atatusaidia sana, ameshaifahamu Ligi ya Tanzania na ameizoea," aliongeza mtoa taarifa wetu.

Chanzo hicho kiliongeza Ihefu ilimwongezea mkataba mpya Januari 24, mwaka huu

INAENDELEA UK. 23

# Nyota wa Mazembe atua Yanga

## ●●● Yupo pia beki wa Lupopo, Hersi akamilisha 'dili' na kupokea ugeni...

**Na Saada Akida**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wameendelea kuimarisha kikosi chao kwa kuwanasa nyota wawili wapya raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), ambao ni beki, Chadrack Boka kutoka Saint Eloi Lupopo na winga wa kulia, Phillipe Kizumbi wa TP Mazembe, imeelezwa.

Habari kutoka Yanga zinasema wachezaji hao wameshaingia mikataba ya kuitumikia timu hiyo baada ya Rais, Hersi Said, kwenda DRC hivi karibuni kukamilisha mchakato huo.

Chanzo chetu kilisema kuwa Boka atachukua nafasi ya Joyce Lomalisa, ambaye mkataba wake unafikia ukingoni mwishoni mwa msimu huu.

Kiliongeza usajili wa Kizumbi umefanyika kwa haraka kutokana na mahusiano ambayo yamewekwa kati ya Hersi na Mmiliki wa TP Mazembe, Moise Katumbi.

Chanzo hicho kiliongeza Kizumbi atatumikia Yanga huku kukiwa na mazungumzo ya kubadilishana na mshambuliaji Mzambia Kennedy Musonda.

**"Dili za wachezaji hao limekamilika, Boka atakuja kuchukua nafasi ya Lomalisa ambaye atapewa mkono wa kwaheri na kutoendelea na Yanga kwa msimu ujao, kuhusu Musonda amebakiza mkataba wa mwaka mmoja ataenda TP Mazembe akibadilishana na Kizumbi," kilisema chanzo chetu.**

Taarifa zaidi zilisema uongozi wa Yanga utaendelea kuboresha kikosi chake kwa sababu kinahitaji kufanya vizuri zaidi kwenye mashindano yote watakayoshiriki.

"Yanga inaendelea kujiimarisha, iko vizuri kumpata kila mchezaji aliye kwenye rada zake na sasa ni muda wa kukamilisha mazungumzo ambayo yalishafanyika huko nyuma, hakuna mchezaji anatesajiliwa kwa kukurupuka," kiliongeza chanzo chetu.

Wakati huo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TP Mazembe, Frederick Kitenge, amewasili nchini kwa ajili ya kukutana na viongozi wa Yanga kwa ajili ya kufanya mazungumzo mbalimbali ikiwamo suala la maendeleo ya klabu hizo mbili.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kuhusu usajili wanaendelea na mchakato huo na watafuata mapendekezo yaliyotolewa na Kocha wao, Miguel Gamondi.

"Niwaambie mashabiki wa Yanga kwa sasa wanatakiwa kufurahia ubingwa tukiwa na mechi tatu mkononi, suala la usajili mambo mazuri yanakuja na ukizingatia tumeingia ushirikiano na klabu ya TP Mazembe ya DR Congo, viongozi wao wapo nchini kujifunza na kubadilisha ujuzi," alisema Kamwe.

Naye Mkurugenzi wa Sheria wa Yanga, Simon Patrick, alisema wamepokea ‚ugeni mzito' kutoka TP Mazembe wenye lengo la kujifunza mambo mbalimbali ikiwamo mfu-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >